# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Oktoba 18, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • Na. 0580372

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710





**UPEPO** kampeni za Magufuli kuikumba mikoa ya kaskazini

UKURASA 3



**LISSU** asema akiwa Rais atakuwa tayari kushauriwa, kukosolewa

UKURASA 2

UKURASA 9

# Ugonjwa hatari watikisa vichwa

**Ni** maradhi yasiyofahamika kwa wengi, Muhimbili wapokea watano kila wiki, madaktari bingwa wataja chanzo ... *Endelea uk. 4*



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akimpa pole mmoja wa majeruhi wa vurugu za kisiasa zilizotokea katika eneo la Kwale, Wilaya ya Micheweni Pemba, waliolazwa katika Hospitali ya Micheweni, jana. **PICHA: IKULU**

# NEC yawaonya waangalizi, wasimamizi wa uchaguzi

UKURASA 2 & 5

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**TCRA YATAJA SABABU WANAWAKE KUONGOZA KUDHALILISHWA MTANDAONI**

MAMLAKA ya Mawasiliano (TCRA), imesema wanawake wanaongoza kwa...

**UKURASA WA 5**

**JK ASEMA HAWAKUFANYA KOSA KUMPITISHA JPM**

RAIS mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, amesema Chama Cha Mapinduzi...

**UKURASA WA 8**

**UMUHIMU WA KUTAMBUA HAIBA KUIMARISHA NDOA**

KATIKA ndoa na uhusiano kuna sifa na tabia ambazo husaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha ndoa na uhusiano. Haiba...


**Mwanafunzi ajinyonga kwa madai ya kukaripiwa na mamaye**

UKURASA 3

**MICHEZO** **CHAMA ANA SIRI MOYONI** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK.6**

## TCRA yataja sababu za wanawake kuongoza kudhalilishwa mtandaoni

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Mawasiliano (TCRA), imesema wanawake wanaongoza kwa kudhalilishwa mitandaoni kutokana na kuwa na tabia za kupiga picha zenye utata na kuzituma mitandaoni pamoja na kutumia simu za wapenzi wao kupiga picha za utupu.

Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi na Utekelezaji wa Sheria na Masharti ya Leseni, Dk. Philip Filikunjombe, alibainisha hayo jana wakati akizungumza katika mkutano wa wadau wa habari na wanachama wa Chama Cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Dar es Salaam (DCPC).

Alisema takwimu hizo ni kwa mujibu kesi wanazopokea katika mamlaka hiyo ambazo nyingi zinawahusu wanawake kudhalilishwa mitandaoni.

"Wanaodhalilishwa mitandaoni, dada zetu wanaoongoza kwa sababu wanapenda kupiga picha na ni wachangiaji wakubwa wa masuala binafsi mitandaoni.

"Changamoto ya usumbufu wa picha zao kuchapishwa na watu wengine mitandaoni inawakuta kwa sababu ya tabia ya kutuma picha mitandaoni," alisisitiza Dk. Filikunjombe.

Aliendelea kutolea mfano kuwa waathirika wa matukio hayo wanapofika TCRA kutaka hatua zichukuliwe dhidi ya waliofanya uhalifu huo, hubainika kuwa walihusika kuzichapisha wenyewe.

"Unakuta dada aliweka picha kwenye mtandao kupitia ukurasa wake na labda wakati huo alikuwa na mpenzi wake ambaye wameshaachana na pengine yeye anatakiwa azifute, lakini anakuwa hakumbuki nywila ya kuingia kwenye ukurasa wake," alisema.

Alisema suala hilo pia linachangiwa na ugawaji wa nywila kwa watu wa karibu au wapenzi wao na tabia ya kupiga picha za utupu au kuzipokea na kuzihifadhi kwenye simu.

Aliwataka Watanzania kuepuka kutuma picha za udhalilishaji mitandaoni kwa sababu ni kosa kisheria na ili kuepuka usumbufu kwa sababu teknolojia imekua na picha inavyotumwa ni rahisi watu kuichukua na kuihifadhi.

## Tundu Lissu: Nikiwa Rais nitakubali kukosolewa

**Na Romana Mallya**

MGOMBEA Urais, Tundu Lissu (CHADEMA), amesema akichaguliwa kuongoza nchi, atakuwa tayari kukosolewa na wananchi.

Amesema kuna haja wananchi kutumia siku 10 zilizobaki kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu, kujipanga kuchagua rais atakayewapa uhuru wa kumkosoa.

Lissu aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wilayani Manyoni mkoani Singida katika mkutano wake wa kampeni.

Akihutubia wananchi hao, mgombea huyo alisema: "Mkapige kura mpate uhuru wa kuwasema hao mnaowapa uongozi. Wakikosea, wasemwe, wakifanya makosa ya kihalifu, washughulikiwe, mkapige kura za haki."

Lissu alisema akipewa ridhaa hiyo, atatengeneza serikali itakayoangalia shida za wananchi kuwa kuwa hiyo ndiyo maana ya maendeleo ya watu.

"Ninawaomba wananchi wa Manyoni muwapigie kura madiwani wote 18 wanaogombea nafasi hii kwa tiketi cha CHADEMA, tukishinda 10 tunaunda Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni," alisema.

Mtaalamu huyo wa sheria alidai wananchi wakiwachagua wabunge wa chama tawala, wakiingia bungeni huingiwa na hofu ya kuisema serikali.

Aliahidi kwenye mkutano huo kuwa akiwa Rais, atahakikisha Bunge linakuwa huru.

Mgombea huyo akiwa mkoani Tabora, alizungumzia kilimo cha tumbaku akisema badala ya kutoa neema kwa wananchi, kimekuwa kilio.

"Ili tutatue tatizo hili la bei ya tumbaku ambayo kwa sasa Tabora bei ya soko kwa kilo ni Sh. 200, tutashughulikia tatizo la kodi, tuwapunguzie kodi wanaonunua tumbaku kwenye viwanda.

"Tukiwapunguzia, hawatakuwa na mzigo mkubwa, tutawaambia wakanunue tumbaku kwa bei ya faida kwa mkulima," alisema.

Lissu alisema wasipofanya hivyo, zipo nchi zinazolima zao hilo na kuzitaja baadhi kuwa ni Malawi na Zimbabwe ambazo alidai kwa sasa zinauza zaidi tumbaku.

"Watakimbia hapa na kwenda kwenye hizo nchi nyingine, wakikimbia na viwanda vyao watakimbia na ajira za vijana wetu, CHADEMA itashughulikia matatizo ya mfumo wa kodi," alisema.

Lissu alisema CHADEMA itaweka utaratibu wa kulipa ruzuku kwenye mazao badala ya kupeleka fedha za serikali katika pembejeo peke yake.

Alisema agano lao na wakulima nchini ni kupunguza mzigo wa kodi wa wanunuzi ili kuwezesha bei ya mazao kama tumbaku kupanda.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akizungumza katika kikao cha utiaji saini hati za makubaliano ya kuondoa hoja tano za muungano zilizopatiwa ufumbuzi, ikiwamo ushirikishwaji wa SMZ, kwenye masuala ya Kimataifa na Kikanda na Biashara, kilichofanyika Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**

## NEC: Waangalizi wasiwe wasemaji wa uchaguzi

**Na Christina Mwakangale**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imewataka waangalizi wote wa uchaguzi mkuu wa mwaka huu waliopata vibali, kutambua kuwa wao siyo watendaji bali wana jukumu la kutazama uchaguzi utakavyokuwa.

Mjumbe wa tume hiyo, Asina Omary, alitoa kauli hiyo alipofungua mafunzo kwa watazamaji wa ndani wa uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28 mwaka huu kutoka Kituo cha Kimataifa cha Sera barani Afrika (CIP) jijini Dar es Salaam jana.

Asina alisema watazamaji hao wanapaswa kukumbuka kuwa wao siyo watendaji wa uchaguzi bali wajibu wao ni kutazama tu namna ambavyo shughuli nzima zinavyoendeshwa, ili kupata fursa ya kuandaa ripoti katika taasisi zao na kutoa mapendekezo mbalimbali. "Kutazama uchaguzi ni jambo ambalo lipo kwa mujibu wa sheria za nchi yetu, hivyo leo (jana) tumeamua kuwakumbusha majukumu ya kazi ili mwisho wa siku wahakikishe wanatazama vizuri uchaguzi huu ambao ni muhimu kwa Watanzania katika kupata viongozi bora watakaowaletea maendeleo," alisema.

Asina alisema NEC mpaka sasa imeshatoa vibali kwa taasisi na asasi 97 za ndani na 17 za nje kwa ajili ya kutazama uchaguzi huo.

"Tunaendelea kutoa vibali vya taasisi mbalimbali zinazotaka kutazama uchaguzi kwani kwa mujibu wa sheria, watazamaji wanaruhusiwa kuwapo na kwenda kwenye kampeni za vyama mbalimbali vya siasa, kujitambulisha kwa wasimamizi wa uchaguzi, kuingia katika chumba cha kupigia kura kuangalia uchaguzi, kuhesabu kura pamoja na majumuisho ya kura hizo.

"Niwakumbushe tu watazamaji wa ndani wana fursa nyingi za kuangalia kwa uzuri na umakini uchaguzi huu kwa sababu wanaijua nchi yao na lugha kwa ufasaha kuliko wale wanaotoka nje ya nchi," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya CIP, Profesa Rwekaza Mukandara, alisema wanaishukuru NEC na Tume ya Taifa ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kwa kutoa vibali vya watazamaji wa kituo hicho ambao kazi yao itakuwa kuangalia mwenendo mzima wa uchaguzi nchini.

Alisema wanatoa mafunzo kwa watazamaji hao ili kuhakikisha wanakwenda kuifanya kazi hiyo kwa mujibu wa sheria, wawe waadilifu na makini pasipo kuegemea upande wowote.

"Tunataka watazamaji wetu wahakikishe kwamba wanachokiona ndicho watakachokitolea taarifa ili hatimaye tuweze kutoa ripoti ambayo ni sahihi na itakayoonyesha kwa ukamilifu yale yaliyojiri, yatufanya tuweze kuamua kama uchaguzi huu ulikuwa huru na haki," alisema Profesa Mukandara.

Mkurugenzi wa Programu kutoka CIP, Raymond Maro, alisema kituo hicho kimeingia kwa mara ya kwanza kutazama uchaguzi mkuu na kuchukua watazamaji 93 ambao watapelekwa Zanzibar na katika mikoa 17 ya Tanzania Bara.

Alisema baada ya mafunzo hayo, watazamaji hao watakwenda kukaa katika mikoa hiyo na wengine Zanzibar kwa takribani siku 10 kwa lengo la kutazama uchaguzi kulingana na sheria inavyotaka.

HABARI KITAIFA

# Serikali yafanya utafiti wa mahitaji vivuko

**Na Richard Makore,** MWANZA

SERIKALI imesema imetuma watalaamu nchi nzima kuzunguka na kufanya utafiti ili kubaini mahitaji halisi ya vivuko, ili ivinunue badala ya kusubiri wananchi waseme.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elius Mwakalinga, alibainisha kuwapo kwa mkakati huo alipozungumza na waandishi wa habari jijini Mwanza juzi.

Alikuwa anazungumzia kuanza kazi kwa kivuko kipya cha MV Ukara chenye uwezo wa kubeba abiria 300, tani 100 za mizigo na magari 10, ambacho kimenunuliwa na serikali, kikitengenezwa na Kampuni ya Songoro Marine Limited.

Alisema kivuko hicho kilinunuliwa kwa gharama ya Sh. bilioni 4.2/- na kitapelekwa Kisiwa cha Ukara kwa ajili ya kuwasaidia wananchi eneo hilo.

Mwakalinga alisema baada ya utafiti huo, timu itakaa pamoja na kuainisha maeneo yenye uhitaji wa vivuko ili serikali itatue kero ya usafiri.

Aliongeza kuwa mpaka sasa, kuna vivuko 31 na kati yake, 16 vinatumika katika Ziwa Victoria na kwamba mwaka huu pekee wamepanga kununua vingine vitatu ambavyo ni MV Chato, MV Ilemela na MV Ukara.



Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, Kheri James (kulia), akimnadi Mgombea ubunge wa jimbo la Arumeru Magharibi, Noah Saputu, katika mkutano wa kampeni uliofanyika Kata ya Kiranyi, Halmashauri ya Arusha DC, juzi. **PICHA: WOINDE SHIZA**

# Upepo wa JPM kutikisa kaskazini

**Na Gwamaka Alipipi**

MGOMBEA Urais, Dk. John Magufuli (JPM), anatarajia kuendelea na kampeni ya duru la mwisho katika Mkoa ya Pwani kisha kuhamishia makali katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Dodoma.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Taifa, Humphrey Polepole, aliyasema hayo jana jijiji Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mambo mbalimbali.

Polepole alisema kuwa Oktoba 19, mwaka huu, Dk. Magufuli ataanza kufanya kampeni za awamu ya mwisho katika Mkoa wa Pwani na baadaye atatikisa mikoa ya kaskazini mwa nchi.

"Siku ya terehe 19 (kesho), mgombea wa urais wa CCM, ataendelea na kampeni, atakuwa Mkoa wa Pwani, ataenda Tanga, Kilimanjaro, Airusha, Manyara, Dodoma, mgombea mwenza Samia Suluhu Hassan kwa sasa yupo Dar es Salaam na atakuwa kwa kazi za kiserikali kisha ataelekea Zanzibar ambako atafanya kampeni Unguja na Pemba, kisha ataenda Morogoro.

"Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Kassim Majaliwa, kwa sasa yupo Dar es Salaam kwa kazi za kiserikali, ataenda mkoani Lindi na Mtwara kufanya kampeni, kwa kweli tumejipanga kuushangaza ulimwengu kwa ushindi wa kishindo," alitamba Polepole.

Polepole pia aliwataka wanachama wa chama hicho kuendelea kufanya kampeni za kistaarabu pamoja na kujitokeza kwa wingi siku ya kupiga kura na kumchagua Dk. Magufuli kuendelea kuongoza nchi.

Vilevile, aliwataka wanachama wa CCM baada ya kupiga kura siku hiyo, warudi nyumbani na kusubiri matokeo aliyoyaita ya kishindo atakayopata mgombea wao huyo.

Alisema kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), pamoja na hukumu iliyotolewa na mahakama, mwananchi akishapiga kura, anatakiwa kuondoka katika kituo cha kupigia kura, wanaoruhusiwa kubaki ni mawakala wa vyama vya siasa pamoja na wasimamizi wa uchaguzi.

"Ushindi wetu kwa mwaka huu utakuwa mkubwa na haujawahi kutokea, mtaji wetu ni mkubwa sana. CCM kwa sasa tupo milioni 17, mtaji wetu wa ushindi ni asilimia 90," alitamba Polepole.

Alisema kwa miaka mitano, Dk. Magufuli amefanya mambo madogo kwa kuwa yatakayofanyika miaka mitano ijayo ni makubwa zaidi.

Polepole pia aliwaomba Watanzania kuendelea kudumisha amani na CCM itaendelea kuisimamia serikali katika kudumisha amani.

Alisema: "Amani ni jambo la muhimu, CCM itaisimamia serikali kwamba amani ya Tanzania iko imara na madhubuti wakati wote. Walinzi wa amani wa taifa hili ni wananchi wenyewe, asiwatishe mtu. Tanzania 'hatunaga' shari na mtu yeyote."

# Mtoto adaiwa kujinyonga kisa mama kumgombeza

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MTOTO Rahel Yohana (14), mkazi wa Kijiji cha Ngayaki, Kata ya Leshata wilayani Gairo mkoani Morogoro, amekutwa porini akiwa amepoteza maisha kwa kile kinachodaiwa kujinyonga.

Inadaiwa chanzo cha kuchukua uamuzi huo ni kugombezwa na mama yake mzazi kwa kitendo chake cha kurejea nyumbani usiku mnene mara kwa mara.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, aliwaambia waandishi wa habari juzi kuwa binti huyo ni miongoni mwa wahitimu wa darasa la saba mwaka huu katika Shule ya Msingi Njungwa iliyoko wilayani huko.

Alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 15, mwaka huu majira ya saa moja asubuhi, ikidaiwa kwamba binti huyo alikorofishana na mama yake siku iliyotangulia baada ya kugombezwa kuhusu kurudi nyumbani nyakati za usiku.

Kamanda huyo alisema binti huyo alikutwa akiwa amekufa kwa kujinyonga kwa kutumia kipande cha kanga alichokifunga kwenye tawi la mti.

Alisema mwili wa binti huyo tayari umeshafanyiwa uchunguzi na madaktari na umekabidhiwa kwa ndugu zake kwa ajili ya maziko.

Alikemea tabia ya watu wanaofikiri njia ya mkato ya kukabili vikwazo vya kimaisha ni kujinyonga, akiwataka wabadilike na wakubali kukutana na watu na wataalamu wa saikolojia kupata ushauri nasaha.

MAKALA MAALUM

# Ugonjwa hatari usiofahamika kwa wengi watikisa Muhimbili

- Husababisha maradhi mengine
- Hospitali yapokea watano kila wiki
- Madaktari bingwa wataja chanzo
- Matibabu yahusisha kukata utumbo

**Na Mary Geofrey**

KUTOKWA haja kubwa pasi na kutarajia, ni ugonjwa unaosababishwa na kukosa seli kwenye utumbo mkubwa zinazosaidia kusukuma haja kubwa kuitoa ndani ya utumbo.

Wataalamu wa masuala ya tiba za binadamu wanauita 'Hisrschospron's desease'. Ni ugonjwa usiofahamika kwa watu wengi, lakini madaktari bingwa wanabainisha kuwa unawakabili watoto wengi nchini.

Hilo linatokana na takwimu za Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), hospitali kubwa zaidi nchini, kubainisha kuwa kila mwezi kuna wastani wa wagonjwa 20 wanaopokewa huko kwa ajili ya matibabu hayo ya kibingwa.

Daktari Bingwa wa Upasuji wa Watoto katika hospitali hiyo, Zaituni Bohari, anasema ugonjwa huo umeonekana kwa watu wengi kama siyo tatizo kwa watoto nchini bali unachukuliwa kama tabia.

Anasema watoto wengi wamekuwa wakichapwa na wazazi na walimu kwa muda mrefu bila kujua kuwa wanawaonea kwa sababu hilo ni tatizo lilipo nje ya uwezo wao.

"Watoto wengi wanapata shida ya kuchapwa fimbo na wazazi wao na kupewa adhabu shuleni kwa kosa la kujinyea wakati suala hilo lipo nje ya uwezo wao," anasema Dk. Bohari.

Mtaalamu huyo anasema chanzo cha ugonjwa huo ni kukosekana kwa seli katika sehemu ya utumbo mkubwa unaopitisha haja kubwa, hali inayomfanya mtoto kushindwa kuzuia kinyesi kinapokuwa kinatoka.

Anafafanua kuwa kinyesi kikiwa kinashuka kwenye utumbo mkubwa ambao una seli, kinakwama eneo la utumbo ambalo halina seli na hivyo kumfanya mtoto ashindwe kupata choo kwa muda mwafaka.

Dk. Bohari anasema wakati kinyesi kinakamuliwa na kushuka katika eneo la utumbo lenye seli, huwa kinakwama eneo ambalo hakuna seli na hivyo kujirundika eneo hilo.

Anasema kinyesi kinaendelea kujirundika kwa muda mrefu na kusababisha tumbo kujaa na matokeo yake kinyesi kinashindwa kujisukuma kutoka nje na badala yake kuanza kutoka kidogo kidogo.

"Matokeo yake ni kwamba kikianza kushuka kidogo kidogo, mtoto anaanza kuchafua nguo bila kujijua na hivyo kuonekana amejinyea," anasema Dk. Bohari.

Anasema wazazi wengi wanakuwa hawafahamu kama hilo ni tatizo kwa sababu watoto wanakuwa hawapati kinyesi kwa muda mrefu.

Mtaalamu huyo anabainisha kuwa mwanzo wa tatizo hilo ni pale mtoto anapozaliwa, lakini anachelewa kupata kinyesi cha kijani kwa mara ya kwanza ndani ya saa 24 na kupata ndani ya saa 48.

"Wazazi wakishajifungua, tunawaambia watoto lazima wapate kinyesi cha kijani ndani ya saa 24 na wanapochelewa kukipata, ni tatizo.

"Lakini, wazazi wanakaa kimya badala ya kurudi hospitali ili mtoto apatiwe matibabu, wanaanza kushauriana kuwapa maji au mafuta ili kulainisha kitoke na kweli kinatoka," anasema Dk. Bohari.



Dk. Zaituni Bohari

**MATIBABU YAKE**

Dk. Bohari anasema wanapompokea mtoto mwenye tatizo hilo, wanaanza kwa kumpa dawa za kulainisha 'choo' na zingine wanamwekea kwenye mfumo wa haja kubwa.

Anasema mtoto kuwa na tatizo hilo humsababisha kupata homa za mara kwa mara, malaria na kupata choo kigumu kama mavi ya mbuzi.

Anafafanua kuwa baada ya kupewa dawa za kulainisha choo, humtengenezea sehemu ya kutolea haja kubwa eneo la ubavuni kwa ajili ya kujisaidia kwa muda akisubiri kufanyiwa upasuaji mkubwa.

Anasema kuwa katika hatua za awali ya kubaini tatizo, wanakata nyama ya eneo la kutolea haja kubwa kwa ajili ya kupima kujua kama hana seli hizo.

Dk. Bohari anasema baada ya kukata nyama, sampuli hiyo hupelekwa maabara kwa ajili ya kupimwa ili kubaini kama hana seli.

Anasema wakibaini tatizo, wanakata utumbo wote ambao hauna seli na kuunganisha kwa kuvuta utumbo mzuri wenye seli hadi karibu na sehemu ya haja kubwa.

Anasema wakishaunganisha utumbo wenye seli na kuondoa ule mbaya, mtoto anaweza kuendelea kupata haja kubwa kama kawaida bila shida yoyote.

**WAGONJWA 20 KILA MWEZI**

Dk. Bohari anabainisha kuwa kuna wastani wa watoto wanaofikishwa Muhimbili kupata matibabu ya ugonjwa huo kila wiki na kati yao, wawili hufanyiwa upasuaji. Anasema upasuaji wanaofanya kwa watoto ni mkubwa, hivyo hulazimika kuwafanyia upasuaji wawili tu kwa kila wiki ili kutoa fursa za upasuji kwa wagonjwa wa magonjwa mengine.

"Matibabu haya ya mtoto kwa hatua zote yanaweza kuchukua mwaka mmoja hadi kupona kabisa tatizo hili," anabainisha mtaalamu huyo wa Muhimbili.

Daktari huyo anawasihi wazazi 'kutochukulia poa' tatizo la mtoto kukosa choo, hivyo wanapaswa kwenda kituo cha afya pindi wanapoona hali hiyo ili kufanyiwa vipimo vitakavyobaini tatizo.

## HABARI KITAIFA

# Kikwete: Hatukufanya makosa kwa JPM 2015

**Na Enock Charles**

RAIS mstaafu Jakaya Kikwete, amesema Chama Cha Mapinduzi (CCM) hakikufanya makosa kilipomteua Dk. John Magufuli kuwa mgombea wake wa urais mwaka 2015 kutokana kazi nzuri aliyoifanyia nchi katika miaka mitano ya uongozi wake.

Alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano wa kampeni za chama hicho kuwaombea kura wagombea wa nafasi za urais, ubunge na udiwani kupitia chama hicho.

Kikwete, maarufu JK, alisema kuwa mwaka 2015 wakati wa uteuzi ndani ya chama hicho, palikuwa na mvutano mkubwa wa kumpata mgombea sahihi wa kukiwakilisha chama hicho kwa vile palikuwa na wagombea wengi, lakini walifikia uamuzi wa kumteua Dk. Magufuli.

"Mwaka 2015 mvutano ulikuwa mkubwa kweli, watu hawakuamini kuwa katika vikao vile tutatoka salama, wengine waliamini tutatoka vipande vipande na kugawanyika, lakini tulitoka salama na hatukufanya makosa," alikumbusha.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wa CCM chini ya Rais Magufuli, nchi imeendelea kuwa na umoja, mshikamano, amani na utulivu, jambo ambalo ni la kujivunia ikizingatiwa zipo nchi zingine ambazo amani imetoweka na zinasumbuliwa na tofauti za kiimani na kikabila.

Kikwete alisema Dk. Magufuli pia amefanya vizuri katika uboreshaji wa miundombinu nchini kwa kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi iliyoachwa na uongozi wa awamu ya nne, akitolea mfano wa ujenzi wa barabara za juu Ubungo, mradi wa mwendokasi ambao ujenzi wake bado unaendelea kwa awamu ya pili hadi ya tano baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza.

Alisema awamu ya tano pia imejipambanua vyema katika kupambana na rushwa na ufisadi nchini na kusisitiza kuwa rushwa siyo tatizo kubwa kwa sasa nchini kulinganishwa na hali ilivyokuwa hapo kabla, hivyo wananchi waendelee kuichagua CCM.

Kuhusu elimu, Kikwete alisema inatolewa bure kwa ngazi ya elimumsingi na mikopo kwa elimu ya juu inaendelea kutolewa, ikiwa ni utekelezaji wa moja ya ahadi za chama hicho za mwaka 2015.

Kada huyo mzoefu wa CCM, alisema uongozi wa Dk. Magufuli pia umeimarisha mashirika ya umma, akisisitiza kuwa katika kipindi cha miaka mitano, mashirika kama vile TTCL, Shirika la Ndege (ATCL) na Shirika la Reli (TRC) yameimarishwa na hivyo kuifanya nchi kujitegemea katika sekta ya mawasiliano na uchukuzi.



Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (aliyevaa suti nyeusi), akimhoji Imamu wa Msikiti wa Arafa Masjid wa Bomang'ombe, Juma Abdalah, kuhusu tukio la kuchomwa moto bweni la chuo cha Quran cha Othuman Bin Halfan, lililokuwa likitumika kulaza wanafunzi 88, wakati kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hiyo, ilipotembelea eneo tukio, jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# NEC yaonya wasimamizi uchaguzi

**Na Romana Mallya**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imesema msimamizi yeyote wa uchaguzi atakayesababisha matokeo kutenguliwa na mahakama baada ya uchaguzi, atalipa fidia za hasara zitakazojitokeza.

Makamu Mwenyekiti wa NEC, Jaji Mbarouk Salim Mbarouk, aliyasema hayo jana katika kikao kilichojumuisha waratibu na wasimamizi wa uchaguzi mikoa ya Kanda ya Kaskazini ambayo ni Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga.

Akizungumza katika kikao hicho, Jaji Mbarouk alisema msimamizi asipozingatia maelekezo ya tume na kuisababishia serikali hasara ya kurudia uchaguzi, atatakiwa kufidia hasara hiyo.

"Atafidia hasara kwa mujibu wa kifungu cha 89(b) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura 343 na kifungu cha 88(b) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Sura 292," alisema.

Kiongozi huyo wa tume alisema tume haitasita kumchukulia hatua msimamizi wa uchaguzi atakayefanya kwa makusudi vitendo vitakavyoharibu uchaguzi.

Jaji Mbarouk alisema Oktoba 28 ndiyo siku ya kupiga kura, hivyo vituo vinatakiwa kufunguliwa kuanzia saa moja asubuhi kama inavyoelekezwa na tume.

"Watendaji wa vituo waelekezwe kuwahi ili wafanye maandalizi na baada ya wapigakura kupiga kura, wanatakiwa kuondoka vituoni.

"Niwakumbushe kwa kuzingatia kufungu cha 89(a) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 na kifungu cha 88(a) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Sura 292.

"Tume haitasita kumchukulia hatua msimamizi yeyote atakayefanya kwa makusudi vitendo vitakavyosababisha uchaguzi kuharibika katika jimbo au kata," alionya.

# Mbaroni kwa tuhuma kujifanya tabibu, kuua

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera, linamshikilia Frodius Protace (24), mkazi wa Kijiji cha Rushe, wilayani Kyerwa kwa tuhuma za kujifanya daktari na kumtoa mimba Saraiya Idd (25) kulikosababisha kifo.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, alisema mjamzito huyo alikuwa ni mkazi wa Kijiji cha Mabuye wilayani Missenyi.

Alisema kuwa baada ya daktari huyo kugundua kuwa amefariki dunia, alikwenda kumzika katika shamba la Anastella Jacob wa Kijiji cha Kisha.

Alisema kaburi la marehemu liligunduliwa na mmiliki wa shamba hilo Oktoba 12 mwaka huu, ambaye alitoa taarifa polisi na baadaye kwenda kufukuliwa.

"Kaburi lilipogundulika na mwili kufukuliwa, marehemu hakutambuliwa haraka na tukio hilo liliripotiwa polisi kama kifo cha shaka kwa sababu ya kutotambuliwa, lakini pia mwili wake kukutwa na dalili ya kutolewa mimba," alisema.

Kiongozi huyo wa polisi alisema mwili huo pia uligundulika kutokwa na damu nyingi sehemu za siri na kuwekwa pamba puani na kuwa dalili hizo ziliibua shaka kubwa ya kifo hicho.

Alisema awali haikufahamika mtu au watu waliohusika kufanya kitendo hicho, lakini uchunguzi wa kina ulipofanywa na jeshi hilo, ulipata taarifa za mtuhumiwa aliyehusika na kumkamata Oktoba 14, mwaka huu.

Alisema ulipofanyika upelelezi katika makazi yake na katika hatua ya mahojiano alikiri kuhusika na kudai kwamba yeye siyo daktari na hajawahi kuhudhuria mafunzo yoyote ya taaluma hiyo.

"Badala yake alisema alihudhuria kozi fupi ya ufamasia lakini hajawahi kuajiriwa serikalini au katika taasisi yoyote ya mtu binafsi," alisema.

Alisema katika chumba cha daktari huyo, wakati wa upekuzi kulipatikana vielelezo mbalimbali ikiwamo matandiko ya kitandani yenye damu, kitambulisho cha mpigakura cha marehemu ambacho kina taarifa binafsi kuhusu marehemu.

"Alikiri kufanya tukio la kumtoa mimba mama huyo yenye umri wa miezi sita, nyumbani kwake akiwa peke yake, kwa malipo ya Sh. 600,000," alisema.

Kwa mujibu wa kamanda huyo, jalada la upelelezi liko ukiongoni ili lipelekwe Ofisi ya Mashtaka kwa ajili ya kuandaliwa mashtaka na kufikishwa mahakamani.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Tume Amani ipongezwe imewakumbusha jambo la muhimu Watanzania*

**KAMATI** ya Amani ya Kitaifa Zanzibar, juzi ilikutana na kufanya mazungumzo na mgombea urais wa Zanzibar kupitia ACT- Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, ikiwa ni hatua ya kujadiliana juu ya umuhimu wa amani katika kipindi hiki cha kampeni na baada ya uchuguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Katika kikao hicho kilichofanyika nyumbani kwa mgombea huyo, Chukwani, Zanzibar na kudumu kwa takriban saa moja, kilihudhuriwa na wajumbe wa kamati hiyo wakiongozwa na mwenyekiti wake, Salum Muhammed na ndiye aliyeongoza mazungumzo hayo.

Viongozi wengine waliohudhuria kikao hicho ni pamoja na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Askofu Michael Hafidhi wa Kanisa la Aglikana Dayosisi ya Zanzibar, Katibu wa Kamati Sheikh Fadhil Suraga na wajumbe kutoka Kanisa Katoliki na kiongozi wa dini ya Kihindu.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, kamati hiyo imeamua kukutana na wagombea wa nafasi ya urais Zanzibar na wadau wengine wakiwamo viongozi wa vyama vya siasa ili kuwakumbusha umuhimu wa kuzingatia amani wakati wa kampeni, kabla na baada ya uchaguzi mkuu.

Jambo la kufurahisha zaidi ni kwamba kiongozi huyo wa kamati alisema mazungumzo baina yao na mgombea huyo yalikwenda vizuri na kukubaliana kuna umuhimu wa kuendelea kukutana na kubadilishana mawazo kuhusu amani.

Pamoja na kukubaliana huko na kufanya mazungumzo, jambo ambalo liliibuka ni umuhimu we kuwapo amani, Maalim Seif akasisitiza kwamba hakuna amani bila ya haki. Kutokana na hali hiyo, aliwataka viongozi na watendaji wenye dhamana ya uchaguzi kuhakikisha wanaheshimu haki ili kudumisha amani.

Ni ukweli usiopingika kwamba amani ni moja ya tunu muhumi kwa taifa ambazo hazina budi kulindwa na kuenziwa kama mboni ya jicho. Kuwapo kwa amani ndiyo msingi wa watu kuishi bila matatizo na kufanya kazi zao kwa utulivu. Viongozi wa kamati ya amani, kutokana na kubuni wazo la kukutana na viongozi wa kisiasa na wanaogombea uongozi hasa urais, wanapaswa kupongezwa kwani wameona umuhimu wa Watanzania kuendelea kuishi katika amani, utulivu, umoja na mshikamano.


Wakati muda wa kampeni ukiwa umebaki mfupi, ni vyema viongozi hao wakakutana na wagombea urais wa Muungano na Zanzibar ili kuliweka sawa suala la amani ambayo ndio kiini cha ustawi wa amani ndani ya nchi baada ya uchaguzi mkuu.

Wagombea na kamati katika vikao vyao, hawana budi kutambua kwamba uchaguzi utapita lakini Tanzania itaendelea, hivyo amani ni muhimu. Kwa maana hiyo, hata lugha zinazotumika kwenye majukwaa ya kampeni zibebe taswira halisi ya maisha na utamadunia wa kitanzania ambao hauna historia kuwa na watu wenye tabia ya kutukanana hadharani wala kuumizana kwa sababu za kidini, kisisasa wala rangi.

Sambamba na wagombea na kamati ya amani, Watanzania pia watambue kwamba maisha yenye amani ni muhimu kwa ustawi wa kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kwa mantiki hiyo kila Mtanzania anatakiwa kutambua kwamba amani ni jambo la muhimu ndani ya taifa.

Kwa mantiki hiyo, katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu, kila mwananchi mpenda amani anapaswa kujua kwamba mchakato wa uchaguzi ni jambo la mpito kwani baada ya Oktoba 28, watu watarejea katika maisha ya kawaida kwa hiyo amani ni muhimu kila siku. Kwa maneno mengine, kuna maisha baada ya uchaguzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# *Wadau wote wa siasa nchini msichoke kuhimiza amani*

Na Sabato Kasika

**KAMPENI** za uchaguzi mkuu zimeingia ngwe ya lala salama kabla ya kufikia Oktoba 28, ambayo Watanzania watakwenda katika vituo vya kupigia kura kuchagua viongozi watakaowaongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Leo zimebaki siku 10 za kampeni za uchaguzi huo wa nafasi ya urais, ubunge na udiwani, ambazo zitahitimishwa Oktoba 27, kisha itakuwa zamu ya wapigakura kufanya uamuzi.

Wagombea kutoka vyama vilivyojitosa katika uchaguzi huo, wanaendelea kujinadi kwa wapigakura kwenye mikoa mbalimbali nchini ili hatimaye wachaguliwe au watoswe siku ya uchaguzi.

Wakati kampeni hizo zikiendelea, ni vyema wadau wa siasa kwa pamoja wakaongeza kasi ya kuhimiza amani bila kuchoka kipindi hiki ili yote yanayoendelea yahitimishwe vizuri.

Kila mmoja ni muhimu akatambua kuwa baada ya hekaheka zote zinazoendelea ni lazima maisha yaendelee, hivyo wadau wa siasa kuanzia Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, wapigakura, viongozi wa dini na wengine kila mmoja afanye kwa sehemu yake.

Amani ni muhimu wakati huu wa kampeni na hata kwenye uchaguzi mkuu kwa sababu bila amani inawezekana watu wasijitokeze kushiriki katika uchaguzi. Ni vyema iwe amani kwanza mengine baadaye.

Suala la amani ni muhimu kwa kuwa kumekuwapo na taarifa za baadhi ya watu kuumizana wakati huu wa kampeni, hali ambayo inatakiwa kukemewa na wadau wote ili zifanyike kwa utulivu.

Amani ikiwapo Watanzania watajitokeza kuchagua viongozi wanaowataka lakini isipokuwapo, wanaweza kuhofia usalama wao wakaacha kujitokeza katika vituo vya kupigia kura Oktoba 28.

Pia hatua ya kuhimiza amani umoja na mshikamano vilivyopo nchini, itasaidia kuwafanya Watanzania waendelee na shughuli zao kwa uhuru bila vurugu na kujiletea maendeleo, kwa manufaa ya vizazi vilivyopo na vijavyo.

Kuvunjika kwa amani kunaweza kuwa kazi rahisi lakini kuirudisha ni vigumu, hivyo wadau wote wa siasa washiriki kikamilifu katika jambo hili kwa kuwahimiza wanasiasa kutambua tunu hiyo iliyopo nchini.

Si vibaya kuwaambia wanasiasa kuwa wawe makini katika kampeni zao kwa kuepuka kutoa lugha za matusi, kuudhi na badala yake wajikite katika kutangaza ilani za sera zao ili kushawishi wapigakura wawachague.

Binafsi, ninaamini kwamba mgombea anaweza kuchaguliwa bila kutukana au kutumia lugha mbaya dhidi ya mwenzake kwa kuwa kwenda kinyume cha hayo ni sawa na kuamsha hasira za watu na kusababisha amani ivurugike.

Suala la kuhimiza amani liwe kama wimbo midomoni mwa wadau wote wa siasa ili kubadili mtazamo wa wanasiasa ambao wanategemea matusi ama lugha chafu kama mtaji dhidi ya wagombea wenzao waache.

Wagombea wanatakiwa kuwashawishi wapigakura wenye sifa ya kupiga kura ili siku ikifika wafanye uamuzi wao kwenye sanduku la kura kuchagua rais, wabunge na madiwani kwa utulivu.

Lakini kwa upande mwingine, vijana nao wanatakiwa kuwa makini na kukataa kutumiwa vibaya na wanasiasa, kama ambavyo Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, amewahi kuwatahadharisha.

Si vibaya vijana kuingia kwenye siasa, kwa kuwa ndiyo viongozi wa taifa la kesho na wana nafasi ya kuandaliwa vyema kwenye ulingo wa siasa badala ya kutumika kufanya vurugu kwa manufaa ya wanasiasa.

Wakati huu ambao Tanzania inaingia katika uchaguzi wa sita ndani ya mfumo wa vyama vingi, ni muhimu kuendelea kuweka suala la amani mbele, kutokana na kuwapo kwa taarifa za baadhi ya watu kuumizwa katika kampeni.

Taarifa za aina hiyo si dalili njema, ndiyo maana nguvu za pamoja za wadau wa siasa, zinahitajika kwa ajili ya kuhimiza amani, ili vijana ambao ndiyo wanaodaiwa kutumiwa vibaya na wanasiasa waache.

000

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Barua kwa Mwalimu Nyerere (RIP)



Nkwazi Mhango, Canada

SHIKAMOO baba. Ni miaka 21 ya machungu na upweke, kama watu na taifa, tangu ututoke. Japo ulitutoka kimwili, kiroho na kiakili bado tuko nawe kama ambavyo tutakuwa nawe hadi tutakapokutana huko uliko. Katika maadhimisho ya kuondoka kwako baba, leo nina machache ya kukueleza kama ifuatavyo:

Mosi, tangu uondoke, taifa letu limebadilika sana. Nakumbuka wakati ukitutoka, ulimuacha kijana wako, ambaye naye amekufuata ghafla mwaka huu, Benjamin W. Mkapa. Baada yake, alikuja kijana mwingine Jakaya Kikwete, ambaye sasa ni mzee na mstaafu pamoja na mrithi wako mzee Ali H. Mwinyi, ambaye bado anadunda.

Muhimu, baada ya Kikwete kuondoka, alichaguliwa kijana mwingine machachari aitwaye John Pombe Magufuli. Kijana huyu, amefanya maajabu hasa kutekeleza yale ambayo ulitaka yatekelezwe. Je unaweza kuamini kuwa makao makuu ya chama na nchi yalishahamia Dodoma huku Dar es Salaam ikirembeshwa utadhani Ulaya.

Wale waliokuwa wakililia kwenda kuona maajabu huko sasa wanakwenda Dar.

Pili, kama haitoshi, lile shirika la ndege uliloanzisha mafisi, mafisadi na wezi wakalifilisi sasa linadunda. Mwaka jana Magufuli alinunua ndege 11 mpya na nane kati ya hizo zimo zinapaa nje na ndani ya nchi. Bila kungoja, kwa sasa kuna meli kibao zinatengenezwa hadi moja kubwa ya kwenda Comoro.

Cha mno, ule mradi mkubwa wa umeme wa mto Rufiji sasa umo mbioni kujengwa. Kwa heshima na kumbukizi lako, umepewa jina lako sambaba na daraja la kuunganisha Feri na Kigamboni. Mambo ya kukatika na migawo ya umeme sasa historia.

Kama haitoshi, je wajua kuwa kwa sasa tupo tunajenga reli mpya ya kisasa ya kutumia umeme ya SGR toka Dar hadi Kigali? Reli za zamani, viwanja vya ndege na madaraja vikikarabatiwa ukiachia mbali ujenzi wa barabara kibao nchini. Siku hizi, kwa mfano, kwenda Kusini kuliko kuwa kumeshindikana ni kama unalia. Mwalimu, kabla ya kusahau, rafiki yako Nelson Mandela, alishaondoka kadhalika Robert Mugabe pia huku mama Maria, akiendelea kudunda japo umri unasogea. Kwa upande wa watoto wako, bado wanaishi maisha ya kawaida sawa na sisi wengine.

Tatu, Mwalimu unaweza kuamini kuwa ule wizi ma mali zetu chini ya ujambazi uitwao uwekezaji umeshakomeshwa? Madini yaliyokuwa yakitoroshwa usiku na mchana sasa yananufaisha taifa kiasi cha kujenga miradi hiyo tajwa bila kukopa kopa, kuomba omba wala kujidhalilisha kama ilivyo kwa mataifa mengi ya Kiswahili. Kule Mirerani yanakopatikana madini ya tanzanite sasa hali ni shwari baada ya eneo lote la machimbo kuzungushiwa ukuta huku kampuni nyonyaji za kigeni zichimbazo madini zikiingia mikataba upya. Kabla sijasahau, siku hizi mashirika na kampuni yanalipa mrahaba wa serikali kama hayana akili nzuri.

Tatu, Mwalimu unajua kuwa lugha ya Kiswahili sasa imekuzwa kiasi cha mataifa ya nje kuanza kuitumia na kuionea fahari. Kwa taarifa yako, sasa Kiswahili kinatumika kwenye SADC na Umoja wa Afrika.

Nne, kama ilivyokuwa wakati wa utawala wako adhimu, kwa sasa, afya na elimu hutolewa bure kwa Watanzania wote bila kubagua chama wala dini. Kama haitoshi, ukusanyaji kodi umeongezeka kiasi cha taifa kuwa na fedha yake ya kutekeleza miradi mikubwa kama nilivyokutajia hapo juu na kutoa huduma za kijamii bure ukiachia mbali kujenga hospitali, zahanati na kukarabati miundombinu ya zamani.

Tano, wale waliozoea kughushi au kuajiri watumishi na wanafunzi hewa walishafyekwa zamani. Kijana Magufuli amebana matumizi hadi wasioelewa somo kulia kuwa vyuma vimebana. Ule wakati wa mchovu kulala maskini na kuamka tajiri ushapita zamani. Kila mtu anakula jasho lake na kuheshimu jasho la wenzake. Wale waliozoea kuibia umma sasa wanalia na ni apeche alolo yaani hawana majivuno ya ukwasi kama zama zile za kiza.

Sita, cha mno, chama chako kipenzi cha Mapinduzi kilichokuwa kimeanza kugeuka chama cha ulaji sasa kimenyooshwa kweli kweli. Mali zake zimerejeshwa mikononi mwa chama na kinaendelea kukua na kubadilika hakuna mfano.

Mambo ya kugombea na kushinda kutegemea mfuko wa mtu yalishafyekwa na kugeuka historia chafu ya chama. Siku hizi mtu anayetaka kupeperusha bendera yake anachujwa kwa kuangalia uadilifu na utendaji wake wa kazi bila kusahau uzalendo. Kwa upande wa upinzani, bado upo unadunda.

Kabla ya kusahau, Watanzania wameongezeka kiasi cha kufikia milioni 50 na ushei huku Muungano ukizidi kuimarika na kulindwa kwa nguvu zote.

Mwalimu, barua hii haitaleta maana kama itaisha bila kukufahamisha kuwa Tanzania sasa ni imara kijamii, kisiasa na kiuchumi kuliko wakati wote wa uhai wake. Misingi uliyoweka sasa inatumika kujenga uchumi hadi kuingia uchumi wa kati mwaka huu miaka mitano kabla ya wakati uliokuwa umekadiriwa. Watu wanachapa kazi kama hawana akili nzuri.

Mwalimu, naomba nisikuchoshe. Kwa leo, ni hayo tu japo yapo mengi ya kufurahisha. Pumzika mahali pema peponi Mwalimu.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Hebu Taifa Stars tuikalie kikao



Na Joseph Kulangwa

WATANZANIA kweli tuna bahati ya mtende. Covid-19 AKA Uviko-19 imetukimbia kama ilivyokuja? Kwa kweli Mungu ashukuriwe kwa hilo na tuendelee kuomba mgeni huyo asirudi tena kutusumbua.

Mnakumbuka tulivyotumbuka macho baada ya kusikia umeingia nchini na watu wanaaga dunia? Mnakumbuka tulivyofokewa kwa kutovaa barakoa? Mnakumbuka tulivyofakamia malimao na kutafuna tangawizi kama ngedere?

Mnakumbuka tulivyojifukiza majani ya miti ya aina mbalimbali bila kujali yana upupu au la? Kisa Uviko aishilie mbali? Mnakumbuka viongozi kila kukicha walivyojitokeza kutufundisha hata kunawa? Fikiria hata kunawa tunafundishwa mizee mizima!

Yaani, mpaka tulifundishwa kutorudia kuvaa nguo? Tukafundishwa kufua nguo? Ukiivaa usiirudie! Maisha haya, kumbe tunaweza kunawa, kumbe tunaweza kuvaa nguo safi. Kwa kifupi tukiamua kujikinga tunaweza, kazi ni kukumbushana tu.

Ukiliona sakata la Uviko ndipo utaona kumbe mengine tunafanya makusudi tu tunaweza kuyaepuka. Tunaweza hata kuepuka kwenda jela, basi tu akili zetu tunazijua wenyewe Wabongo. Lakini Uviko ilitufunza adabu.

Tulikaa bila shule, tulikaa hatuendi kuangalia burudani, wenye kiu hatukwenda baa, maanake kila mahali Uviko alitamalaki. Lakini sasa alhamdulilahi. Michezo imeanza tunashuhudia ligi zetu, watu wanafurika viwanjani. Kubwa kampeni zinashuhudia nyomi bila barakoa.

Tuna michezo ya Kombe la Mataifa ya Afrika imeanza, nasi tunashiriki, kama kawaida tunaangalia tutakachokivuna baada ya kukaa bila kucheza kutokana na Uviko. Tumeunda timu yetu ya Taifa, kama kawaida si ya kudumu sana kama za wenzetu, kwani sisi huokoteza mashindano yakikaribia.

Hatupendi kufanya hivyo, la hasha, lakini tatizo hatuna wachezaji wengi wa kulipwa kama wenzetu Ughaibuni, ambao wanaweza kuwa na timu ya Taifa tatu hadi nne nje ya mataifa yao.

Kwao ni rahisi kuitana na kukusanyana leo na kesho kutwa kuingia uwanjani kuonesha maajabu. Sisi tutafikria kina Samatta, Msuva, Mao na wengine wawili watatu hivi, waje tuchanganye na walioko hapa ndipo tukashindane.

Hatuna jinsi, lakini kama tutaamua na kujenga wachezaji wetu wa ndani badala ya kuwajazia wa kigeni kwa kisingizo cha eti wapate changamoto, tunajidanganya. Kuna wakati Waziri Harrison (Huyu si Morrison acheni kutoa mimacho), alifungua uwanja wa majidiliano kuhusu wageni 10 kwenye timu zetu, akalemewa na ubishi wa Wabongo, yakabaki hivyo hivyo. Angalia timu zetu kubwa hizi hasa Yanga, Simba na Azam, zilizokithiri wageni, utaona ni hao tu ndio wanaocheza na kufunga huku wa ndani wakibaki kutazama tu. Kisa ni kwamba tunajali timu za klabu zishinde, bila kuangalia hatima ya Timu ya Taifa.

Hivi kama washambuliaji tulionao wazawa ni Bocco na sijui mwingine nani, na huyo hachezi mara kwa mara kwa sababu tuna Kagere na Mugalu, au kama Waziri Junior hachezi kwa sababu tuna Sarpong na Kisinda, Chilunda hachezi kwa sababu kuna Dube na Tigere, ni lini wataisaidia Taifa Stars?

Wageni huku wanajijenga na wakiitwa kwao, wanakwenda kuzisaidia timu zao za Taifa, ninyi ndo kwanza mnakusanyana, kujipanga kukabiliana na timu hizo hizo zenye wachezaji hao hao walioko nchini na wanapewa nafasi kucheza.

Basi kama tumeshindwa kufanya la kufanya, basi nyie TFF, waombeni wageni wote walioko nchini, waunde timu yao ambayo itakuwa ikitumika kuipima nguvu Taifa Stars kila mara ikihitajika kuliko kutumia gharama kualika timu ya Taifa lingine kuja kujipima au kuwafuata kwao kwa lengo hilo hilo.

Kuna wachezaji wa kigeni wanaochezea timu za Taifa ambao ni wazuri na wanaotosha kuipima nguvu Taifa Stars na ikajijenga vema, na hivyo isisubiri michuano kuanza, yaani tunakuwa na timu ya Taifa ya kudumu hata kama ni ya CHAN. Mbona Samatta na Kiba wanaweza na Samakiba yao? Wao wanaweza wana nini na sisi tushindwe tuna nini? Alamsiki.

## KONA YA UKWELI



Na Thobias Mwanakatwe

# Tuchague viongozi wenye uzalendo, utaifa kwa nchi

KAMPENI kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba 28, mwaka huu zinatarajia kuhitimishwa Oktoba 27, ikiwa ni siku moja kabla ya wananchi kushiriki kupiga kura kuchagua viongozi wanaowahitaji.

Wananchi watapiga kura kuchagua Rais, wabunge, wawakilishi na madiwani baada ya kuwachuja na kusikiliza sera walizokuwa wakizinadi kwenye mikutano ya kampeni ambayo ilianza Agosti 28, mwaka huu.

Swali la msingi ambalo tunapaswa kujiuliza wapigakura ni je, wagombea tunaokwenda kuwachagua walionyesha uzalendo na utaifa kwa nchi yao kwenye kampeni zao?

Hili ni swali la msingi kabla ya kuchukua uamuzi wa kupiga kura kwa sababu wananchi tukiingia mkenge tukachagua kiongozi asiyekuwa mzalendo kwa nchi yake, tutarajie kuwa ipo siku tutavuna mabua, kwani kiongozi wa namna hiyo ni hatari.

Kama tunavyofahamu kuwa uzalendo ni hali ya mtu kuipenda sana nchi yake kiasi cha kuwa tayari kufa kwa kuitetea, wakati utaifa ni jumla ya mambo yote ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kisheria yanayowaunganisha watu kuwa nchi moja.

Baada ya kuwa tumewasikiliza wagombea wetu kwenye mikutano ya kampeni ambayo imedumu takribani siku 60, siku ya kupiga kura wananchi wasifanye kosa.

Tukichagua viongozi wenye uzalendo na utaifa tufahamu kuwa hapo tutakuwa tunaiweka nchi yetu katika mikono salama lakini tukichagua wasio na uzalendo tusishangae nchi yetu ikawa koloni tena.

Tufahamu kuwa historia ya uzalendo ilianza wakati wa kupigania uhuru wa nchi yetu ambapo mababu zetu walipigana uso kwa uso na wakoloni kukataa kutawaliwa kwa nguvu na kuchukuliwa rasilimali zao.

Wakati wa harakati hizo, wazee hao waliuawa kwa kunyongwa au kupiga risasi na wengine walifia magerezani ili lengo lao la kupigania rasilimali za nchi zisiweze kuendelea kuchukuliwa na mabeberu.

Nilichokibaini katika kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka huu, wako baadhi ya wagombea wanataka kuirudisha nchi yetu kwa wakoloni ili mabeberu waendelee kunufaika na raslimali zetu zilizopo nchini.

Nayasema hayo kutokana na kauli zinazotokewa na baadhi ya wagombea ambao wanaonekana kubeba agenda za mabeberu kitu ambacho ni hatari sana.

Nchi nyingi za Afrika ambazo zimeingia katika machafuko chanzo chake kimetokana na wanasiasa ambao wanausaka uongozi kwa kutumiwa na mabeberu kwa maslahi yao na lengo lao linaposhindikana wanatafuta njia mbadala kuzusha vurugu.

Wananchi chonde chonde tusitowe nafasi kwa wanasiasa wa aina hiyo, nchi yetu ina historia duniani ya kuwa nchi yenye amani ya utulivu.

Siku ya kupiga kura mwananchi kabla hujachukua uamuzi lazima uyatafakari maneno, kauli, ilani na sera ambazo mgombea husika alikuwa akiyanena kwenye mikutano yake ya kampeni.

Hapa ndipo unatambua kuwa kipindi cha kampeni ni cha muhimu kwa wananchi kuweza kusikiliza sera za wagombea kwasababu hapo ndipo unapata kufahamu mgombea mwenye malengo ya dhati ya kukuletea maendeleo ni nani na anayetumiwa na mabeberu kutaka kuleta vurugu nchini.

Ni matumaini ya kila mwananchi kuwa amepata fursa ya kuwasikiliza wagombea wote, na niwe wazi wako baadhi yao sera na mipango yao inatisha kidogo kwa mustakabali wa nchi.

Wako watu ambao wanadai wao watachagua mtu si sera wala chama kwa kuwa jambo hilo ni uamuzi wa kila mtu lakini kwa mawazo yangu suala la sera na ilani za chama ni la muhimu sana kuzingatiwa siku ya kupiga kura.

Mfano wako baadhi ya wagombea wamesikika kabisa wakitoa maneno ambayo yanaleta mtazamo kwamba siku watakayochaguliwa tu basi vurugu itakuwa ni sehemu ya utawala wao.

Tukumbuke kuwa viongozi tunaowachagua watakuwapo madarakani kwa kipindi cha miaka mitano hadi 2025, kwa hiyo ukifanya makosa itakugharimu muda wote huo.

Watanzania twendeni tukapige kura tukizingatia kuwa tunakwenda kuchagua viongozi sahihi na makini watakaotuletea maendeleo ya kweli na siyo wenye lengo la kuvuruga amani yetu.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**
**MUNGU UBARIKI UCHAGUZI MKUU 2020**

**Kwa maoni na ushauri tuwasiliane Email; mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka
0744000066

# Umuhimu wa kutambua haiba Katika kuimarisha ndoa - 2

KATIKA makala iliyopita, tuliangalia kwa undani sifa na tabia za watu wenye haiba tofauti ambazo zinawatambulisha kwa ni watu wa aina gani. Makundi ambayo yalijadiliwa kwenye makala hiyo ni Melankoli (Melancholic) na Flegmatiki (flegmatich).

Leo tunaendelea kudadavua haiba zingine za watu, lengo likiwa kuwawezesha watu kuwatambua na pia kuimarisha uhusiano wao katika ndoa. Kundi lingine katika utambulisho wa haiba ni Sangwini (Sanguine).

Neno Sangwini maana yake ni -enye furaha. Hili ni kundi la watu wenye hisia za wazi. Si watu wa kutunza mambo moyoni; ni watu wasio na vinyongo kwani raha yao ni kuzungumza pale wanapokosewa.

Kwa kawaida, Sangwini hupendelea watu wa aina yao. Watu hawa hupenda Sangwini wenzao ambao pia ni wacheshi katika masuala yote. Kwa Sangwini, uhusiano wa kimapenzi ni burudani na upendo ni kuwa na mitoko pamoja na kufanya mambo mapya. Si watu wa kukaa mahali pamoja kwa muda mrefu; hupenda safari na burudani. Hawawabani na hawapendi kuwakwaza wenzi wao.

Sifa za ziada za Sangwini ni watu wachangamfu na wazungumzaji sana. Si watunzaji wazuri wa siri kwa sababu ya hali yao ya kupenda kuzungumza sana. Huweza kusema mambo bila kufikiri vizuri. Wana uwezo wa kumzoea mtu ndani ya muda mfupi na ni wepesi kutengeneza marafiki.

Pamoja na sifa hiyo nzuri, Sangwini hupoteza marafiki kwa haraka kwani kutengeneza marafiki wapya kwake si kazi. Ni watu wanaopenda kuchekesha wengine, kwa hiyo mazungumzo yao yanatawaliwa na watu kucheka sana.

Pia wana tabia ya kumpenda mtu kwa haraka sana. Upendo unakua haraka ndani ya moyo wake kiasi cha kuweza kutaka kutangaza uchumba saa hiyo hiyo.

Sangwini ni watu wenye nguvu kubwa ya ushawishi kwa sababu ya uwezo wao wa kujieleza na kutoa ahadi nyingi hata kama hazitekelezeki. Mara nyingi ni wasemaji wazuri kuliko kutenda. Ndiyo maana uhusiano wao wa kiuchumba wakati mwingine hudumu kwa muda mfupi.

Ni watu wanaopenda kusifiwa na kutambulika. Hawa ndio wale watu ambao akifanya jambo anapenda watu watambue na kumsifia.

Mfano, anapotoa msaada kwa watu, anapenda watu wote waone na kumpigia kofi kwa sababu anajisikia raha. Kama ni katika kutambulisha watu, usifanye kosa la kusahau kumtambulisha.

Sangwini ni watu wepesi sana kuomba msamaha wanapokosea, lakini wepesi kufanya makosa ya mara kwa mara. Ni wepesi wa hasira; lakini wepesi wa kusamehe.

Pia ni wepesi sana kusaliti maazimio ya awali. Wengi wao ni wanafiki sana au ndumilakuwili. Hii ni kwa sababu wanapenda kupendwa na watu wote au kuridhisha pande zote. Hawana nidhamu ya fedha wala vipaumbele. Anaweza kununua hata kitu asichokihitaji huku akitambua kuwa bado anadaiwa kodi ya pango. Sangwini hupenda tendo la ndoa mara kwa mara.


Anapokutana na Melankoli wanapenda kutengeneza taratibu njema za kifamilia. Wanaendana katika uhusiano wao kwa sababu ya uwiano wao kwa kuwa Sangwini ni watu wa 'kupanda' wanapokasirika na 'Melankolini ni watu wa 'kushuka'.

Mchanganyiko huo unawafanya waendane na kuepusha mizozo katika uhusiano. Lakini, pia, inapotokea Sangwini akapendana na Flegmatiki inapendeza sana maana wanakuwa na upatanifu. Wote wana hisia za kuhitajiana na wenye kuridhiana.

**Itaendelea Jumapili ijayo**


**■Mchungaji Mlyuka ni Mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Tanzania Mariage and Child Care (TaMCare), inayojishughulisha na masuala ya Ndoa na Malezi ya Watoto. Kwa maoni na ushauri, wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz**

MAISHA
OKTOBA 18, 2020
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



## HARUSI

Ukurasa 12



Ukurasa 10

**Mfunze mwanao apende kusoma vitabu**



## MAISHA NI NYUMBA

Hii ndiyo sebule inayoita

Ukurasa 15



## KABABU ZA NYAMA

Ukurasa 14

# PETE KIFUNDO

## Urembo unaowachanganya

## WENYE FEDHA







Ukurasa 14

# Mfunze mwanao apende kusoma vitabu

**Na Moses Ismail**

NI takribani miaka hamsini sasa tangu uliposoma vitabu vya 'Kusoma' vya darasa la pili na la tatu katika miaka ya 1970 ulipokuwa katika madarasa hayo.
Lakini hadi leo, mwaka 2020, bado unakumbuka vizuri hadithi zote za 'Juma na Roza', 'Damasi na Lusi', 'Manenge na Mandawa', 'Bora mimi sikusema' na nyingine nyingi tu.
Halafu hata kabla ya kufika darasa la nne, unakumbuka kuwa tayari ulishaanza kusoma vitabu vya 'Lugha Yetu', na ndio maana hujasahau hadithi za 'Sikiri na Sadiki, 'Kibanga ampiga mkoni', 'Sizitaki mbichi hizi' na hadithi nyingine nyingi za vitabu hivyo
Achana na kumbukumbu zako za mwaka '47, rejea katika wakati huu tulipo ambao pengine una watoto wakubwa waliomaliza darasa la saba miaka ya 1990 au miaka hii 2000, umewahi kufikiria ni vitabu gani walivyosoma wao kwa wakati wao na wanakumbuka nini juu ya vitabu hivyo?
Mimi nimewahi na majibu niliyojibu yalionyesha hakuna kitabu chochote wanachokumbuka watoto wetu zaidi ya kukumbuka katuni mbalimbali na hii yaweza kuthibitisha kuwa utamaduni wa watoto wetu kusoma vutabu, umekufa.
Hili la kufa kwa utaratibu wa watoto kutopenda kusoma vitabu au hata majarida, lina athari mbaya kwa mfumo mzima wa ufahamu wao hasa kwa kujenga picha za hisia kiakili.
Mfano, unaposoma kitabu, unapata muda wa kujenga hisia mbali mbali, kwa mfano unajenga picha ya wahusika na mandhari na hata umakini wa tukio lenyewe, hapa unasaidia akili yako kutanuka".
Chukulia hadithi ya kitabu inayozungumzia nyoka mwenye vichwa saba, hii inashughulisha akili ya msomaji kumfikiria nyoka huyo wa vichwa saba namna alivyo na kujenga picha yake mwenyewe na kupata aina ya nyoka huyo.
Kinyume na kuangalia sinema au katuni, kwa kuangalia katuni na sinema msomaji hapata nafasi ya kujenga taswira yake kwa sababu tayari watengeneza sinema wameshamchagulia nyoka wao. Unamuona, hushugulishi akili tena.
Selina Gonza, ofisa mshauri wa ustawi wa jamii katika taasisi moja binafsi jijini Dar es Salaam inayoshughulika na masuala ya ustawi wa watoto na elimu anaeleza athari za kutosoma vitabu hasa nchini Marekani ambapo juhudi za makusudi zinafanywa kuwarudisha watu kwenye utamaduni wa kusoma vutabu. Anasema:
"Marekani wamegundua rai wao wengi wanatatizo la ufumbuzi wa mambo kwa sababu ya kukosa muda wa kusoma vitabu na wameshaanza kuweka mikakati ya kuhamasisha watu kupenda kusoama vitabu.
Inawezekana kuwa jamii yetu haijafikia huko kwa sababu televisheni zetu bado zinaonyesha vipindi kadhaa vya elimu ingawa vile vya burudani ni vingi zaidi, lakini wingi wa sinema majumbani mwetu unaweza kutupelekea huko.
Ni vyema basi wazazi kuwapangia watoto muda wa kusoma vitabu vya hadithi na elimu ili kuwanasua na 'mtego' huu wa kuangalia sana sinema na tamthilia kwa kuzingatia kuwa haziwajengi sana kiakili kama kusoma vitabu.

## QUIZ

**NA KHAMIS KIDAGO**
0657 207168

### LE QUIZ DU WEEK

1. Nyumbua kitenzi "Être" kama maelekezo yanavyoonesha hapo chini.

Conditionnel
Présent
Je ..................
Tu ..................
Il/elle ..................
Nous ..................
Vous ..................
Ils/ells ..................

Passé
J' ..............................
Tu ..............................
Il/elle ..............................
Nous ..............................
Vous ..............................
Ils/elles ..............................

2. Nyumbua kitenzi "Être" katika "Infinitif" présent na passé.
- Présent =
- Passé = ..................

3. Weka kitenzi "Être" katika Participe présent na passé.
- Présent = ................
- Passé = ..................
..................

4. Pangilia kitenzi "Être" katika Impératif présent na passé.
- Présent = .............
.............
.............
- Passé = ..................
..................
..................

### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA

Le quiz du week – end
- Nyumbua kitenzi "Être" kama maelekezo yanavyoonesha hapo chini.

Conditionnel
Présent
Je serais
Tu serais
Il/elle serait
Nous serions
Vous seriez
Ils/ells seraient

Passé
J' aurais été
Tu aurais été
Il/elle aurait été
Nous aurions été
Vous auriez été
Ils/elles auraient été


- Nyumbua kitenzi "Être" katika "Infinitif" présent na passé.
  - Présent = être
  - Passé = avoir été
  - Weka kitenzi "Être" katika Participe présent na passé.
  - Présent = étant
  - Passé = été
  ayant été
- Pangilia kitenzi "Être" katika Impératif présent na passé.
  - Présent = sois
  soyons
  soyez
  - Passé = aie été
  ayons été
  ayez été

## WATOTO

## PAKA RANGI




## CHEKA KIDOGO



JAMAA mmoja bahili alimchukua mtoto wake kwenda mjini kutembea, walipofika alikwenda kumnunulia chakula .

**BABA: Chipsi bei gani?**
**MUUZAJI: Elfu mbili**
**BABA: Zina kachumbari, ukwaju na nyanya?**
**MUUZAJI: Ndio!_**
**BABA: Kachumbari peke yake unauzaje?**
**MUUZAJI: Ni bure**
**BABA: Oke, Basi naomba sahani mbili**
**MTOTO: Babaaa!**

**SWALI**
**Mlima mrefu barani Afrika unaitwaje?**

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Unapomkataza mke kufanya kazi kisha unalalamika, unajitambua?

MPENZI msomaji, tunaendelea na vimbwanga vya Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita, tulijadili wale wanaume wanaofanya kazi lakini wake zao kutwa wanazurura mitaani. Huyu si mama aliye bora bali muua hatima ya familia.

Ni muhimu sana maendeleo ya familia, viongozi wake ambao ni baba na mama, wote washirikiana kuyajenga ili matokeo mazuri yaonekane. Hilo ndilo kusudi la familia iliyo bora.

Leo hebu tumjadili Yule mwanamke anayetaka kufanya kazi lakini mumewe badala ya kumtia moyo, anamkatisha tamaa. Kibaya zaidi, mwanamume wa aina hiyo anakuwa kila wakati anamlalamikia mkewe kwamba hachangii pato la familia ila anaponyanyuka kuitafuta hiyo kazi, hampi nafasi.

Yuko mama mmoja baada ya kusoma makala ya wiki iliyopita, alinipigia simu kunielezea misukosuko aliyowahi kupata wakati akiishi na mume wake katika ndoa iliyodumu miaka takribani sita.

Alipokuwa hana kazi, mume alilalamika na alipoitafuta akaipata, akaanza kupigwa vita. Mara mshahara mdogo, umetafutiwa na mabwana zako na maneno ya kuudhi kibao ilimradi kumkatisha tamaa.

Anasema hivi: "Wazazi wangu wamenisomesha kwa gharama kubwa sana hadi ngazi ya chuo kikuu na kujipatia digrii yangu. Sambamba na masomo hayo nikaolewa na kujaliwa kupata watoto wawili.

"Nikawa natafuta kazi ya kuningizia kipato nichangie pato la familia. Cha ajabu, kila wazo la mradi ninalopendekeza nilifanye, mume wangu tunakubaliana lakini katika utekelezaji, ananikwamisha.

"Nikataka nianzishe duka kuuza bidhaa mbalimbali, wazo akaliyeyusha. Nikataka niwe wakala huduma ya M-Pesa, Tigo Pesa na kadhalika.

"Nikapambana nikapata laini kampuni mbili za simu, badala ya kunifungulia fremu nifanye kazi hiyo, zile laini akawa anazunguka nazo huko kazini kwake. Eti ana wateja wengi atawahudumia mwenyewe. Ikabidi niwe mpole, nikatulia.

"Nikataka kupika keki, nikapata mashine ya kuokea nikaanza lakini akanikwamisha njiani. Simu za oda ananiwazia eti ni za mabwana zangu Ikiwa sasa ni kunisimanga eti sina mchango wowote kwake.

"Ilipofikia hapo, nikasema ngoja nitafute kazi yangu mwenyewe kupitia vyeti vyangu nilivyosoma miaka sita. Mungu akanijalia nikapata kazi.Katika hatua hii, vita ikawa kubwa zaidi, eti posho ni ndogo.

"Hapo nilikuwa bado kwenye majaribio sijathibitishwa kazini ili nipewe mshahara kwa mwezi. Ilifikia wakati ananikataza kwenda kazini, nilipoijulisha familia yangu ikamjia juu, akatulia.

"Hata hivyo, kila wakati ananitafutia sababu na kunipiga, wakati mwingine mbele ya watoto wetu wadogo. Tatizo kubwa la bwana huyu ni mkono wa kupiga. Majeraha ya kipigo niliyo nayo yakanifikisha mwisho nikafungua shauri la talaka mahakamani ndoa ikavunjikia mbali.

"Kutokana na kisa hicho, nikawa najiuliza sana kwa nini baadhi ya wanaume huwakataza wake zao kufanya kazi kuchangia pato la familia hasa wanaume ambao bado hawana uchumi mkubwa? Nikasema sitaacha kazi niliyoitafuta mwenyewe hadi kikaeleweka." Hivi ndivyo anavyomalizia mama huyu.

Msomaji wangu, bila shaka umemwelewa. Ni kweli kabisa wako baadhi ya wanaume hawajui umuhimu wa wanawake katika kuchangia la familia. Hawa wana tabia, ikiwamo wivu usio na faida yoyote.

Zaidi ni wale wanaume wasiojiamini katika uamuzi. Hutegemea zaidi ushauri wa marafiki au wazazi, jambo ambalo ni hatari sana. Kuna uamuzi unapaswa kusimama mwenyewe.

Mama huyu anaitambua vyema nafasi yake katika kujiamini ili kujiinua kiuchumi. Pamoja na misukosuko yote hiyo, alijitia nguvu pale aliposema, nitaendelea na kazi yangu hadi kieleweke.

Kujitia nguvu kuna maana nyingi ikiwa ni pamoja na kuvaa ujasiri na kufanya jambo ulilokusudia pamoja na kuwa na moyo wa uhodari na ushujaa kulinda kile ulichokiamini na kusimamia hofu. Pia ni kuwa na tumaini haijalishi ni mazingira gani utapitia lazima utimize kusudi lako.

Kwa nini yakupasa kujitia moyo? Mungu anamthamini kila mmoja wetu na amewekeza vitu vingi ndani yake. Kwa mantiki hiyo, hatupaswi kuvunjana moyo maana anatutegemea.

Kama hutajitia nguvu, utashindwa kutimiza kusudi na majukumu yako kama mwanadamu aliyekamilika. Maisha Ndivyo Yalivyo.

**Bila shaka, msomaji wangu umejifunza jambo hapa. Je, una maoni na kisa tujadili pamoja? Ukiwa tayari, nitumie kupitia 0715268581. Namba hii ipo pia WhatsAAP. Tukutane wiki ijayo.**

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Tufanye uamuzi sahihi Oktoba 28, uchaguzi usitugawe

ZIMEBAKI siku 11 ili kila Mtanzania afanye uamuzi juu ya nani anafaa kuwa diwani wa kata yake ili awakilishe maoni ya wengi katika kikao cha Baraza la Madiwani na kufanya mipango na utekelezaji wa masuala mbalimbali ngazi ya serikali za mitaa.

Oktoba 28, mwaka huu, pia wananchi watafanya uamuzi wa nani anafaa kuwa mbunge wa jimbo lao ambaye atawawakilisha katika chombo cha kutunga sheria na kuisimamia serikali, ambacho ni Bunge.

Aidha, siku hiyo wananchi ndiyo wataamua nani anastahili kuwa Rais wa Tanzania kwa miaka mingine mitano kabla ya kwenda kwenye uchaguzi mkuu mwingine kwa mujibu wa katiba.

Kwa sasa, kampeni ziko katika wiki za lala salama kwa kila mgombea kukamilisha kuwafikia wapigakura kulingana na kalenda iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kila chama kimeweka bayana ilani zake na kimenadi sera zitakazotekelezwa ikiwa watapata ridhaa.

Pia juzi NEC ilikabidhi kwa vyama vya siasa daftari la mfano ikiwamo kuonyesha jinsi karatasi ya kupiga kura itakavyokuwa. Tayari karatasi hiyo imesambaa na kila mpigakura ameona mgombea wake yuko katika nafasi gani.

NEC pia imeweka utaratibu wa kila mpigakura kuhakiki taarifa zake kwa njia ya mtandao na kujua kama kweli anasomeka kwenye daftari na atakuwa na uhakika wa kupiga kura.

Kipindi cha kampeni tangu kura za maoni, mengi yaliibuka ikiwamo baadhi ya watu kupoteza maisha na kujeruhiwa kiasi cha kupata ulemavu wa kudumu. Matukio ya udhalilishaji na kuumiza wengine pia yalionekana kupitia video mbalimbali.

Kwa ujumla, matukio haya yanatia doa uchaguzi na ni lazima vyombo vya dola vihakikishe vinatenda haki kwa kila mchezaji katika uwanja wa siasa. Vinginevyo ni kuacha wananchi na maumivu mioyoni ambayo kutibika kwake ni muda mrefu.

Mathalani, wako walipoteza wapendwa wao, wako wanaosota gerezani na wako walioko hospitalini wakiuguza majeraha na zaidi wanaouguza majeraha ya mioyoni kimya kimya. Wote hao wanahitaji tiba ili kuliponya taifa.

Haki huinua taifa na siku zote kukiwa na haki amani hutamalaki na daima haipendezi na haikubaliki kuhubiri amani huku umeficha silaha ya moto kwapani, bali amani ikihuribiriwa ihubiriwe kweli, itendeke na ionekane kweli imetendeka.

Ni wajibu wetu sote kujenga amani ya nchi kwa kuwa hakuna mwenye hati miliki zaidi ya mwingine wa nchi ya Tanzania, kila mmoja ana nafasi yake kuhakikisha taifa linazidi kustawi badala ya kurudi nyuma na kuwa na doa kitaifa na kimataifa.

Misingi ya utaifa, umoja na amani inapaswa kulindwa kwa nguvu zote, ikiwa inaharibiwa kwa maslahi flani ya wachache maana yake wapo wanaamua wengine waishi na wengine wasiishi, kiasi cha kuwa Mola au Mungu anayegawa pumzi ya uhai kwa wengine.

Yako mataifa yalijikuta vipande vipande kwa sababu tu ya mchakato wa kidemokrasia wa kupata kiongozi wa kuongoza nchi. Lakini wako ambao mchakato huo uliwaimarisha zaidi na kubaki kuwa taifa moja lenye kunia na kunena mamoja.

Hivyo basi, nasi tunapaswa kuziba kila nyufa ambayo inataka kuligawanya taifa kwa misingi ambayo mwasisi wa taifa, Mwalimu Julias Nyerere, alifanikiwa kuikemea na haikuwa na nguvu. Kama tutakubali kugawanywa kwa kwa misingi ya itikadi, dini, ukanda wa nchi, rangi au kabila maana yake taifa linakengeuka, na hali ikiwa hivyo namna ya kutibu itakuwa ngumu zaidi

Naamini kabisa bado tuna nafasi kubwa ya kulijenga taifa katika misingi yake imara, kuponya majeraha yoyote yaliyopo ikiwamo yanayotarajiwa kupatikana kutokana na uchaguzi wa Oktoba 28, mwaka huu, lakini la msingi ni namna gani tutabaki kuwa wamoja.

Kila mmoja kwa imani yake amuombe Mungu ili uchaguzi uwe huru na haki, kwa kuwa siku zote haki huinua taifa na huleta umoja wa kitaifa.

**Mungu Ibariki Tanzania**
**Kwa maoni,Ushauri: salomekitomari33@gmail.com**




Ilikuwa ni siku ya furaha kwa Hariss Mhumbira na Suzan Luanda, walipofunga ndoa katika Kanisa la St. Immaculate Upanga, jijini Dar es Salaam.

# HARISS & SUZAN

# MITINDO



# YA KALE DHAHABU

## Nguo za zamani zinaleta mabadilko

BAADHI ya watu wana tabia ya kuwa na nguo nyingi ambazo hawazivai, badala yake wanazijaza kabatini na mwishowe hugeuka kuwa uchafu.
Katika dunia ya mitindo, kuwa na nguo nyingi ambazo huna matumizi nazo ni sawa na kujiongezea kazi ya kufikiria pale unapotaka kuvaa.
Ni muhimu kuwa na ratiba ya nguo zako na wakati mwingine kufahamu aina ya nguo na siku unayofaa ndani ya wiki au mwezi.
Kama una nguo nyingi, sio lazima uzigawe zote, bali inatakiwa kuziweka katika ratiba zako kwani aina ya mitindo ya zamani bado inaendelea kupendwa.
Nguo zilizotumika na zikachwa kwa muda ni alama nzuri ya muonekano wako mpya, kwani pale utakapovaa unaonekana tofauti na wengine.
Unashauriwa kila nguo ambayo umeitumia uiweke katika mpango wako wa baadae na si kutupa kabatini na kisha kuzitelekeza.
Kwa ujumla mavazi ya zamani ni azina yako, kila nguo hakikisha inakuwa katika malengo yako, kwani si kila nguo hutakiwi kurudia kuvaa.

# UREMBO

## PETE KIFUNDO

# Urembo unaowachanganya wenye fedha

KATIKA urembo, leo tutapeana elimu jinsi ya kuvaa pete za kifundoni kwenye vidole vya mikononi.

Aina hii ya pete zinafahamika kama 'knuckle rings' zinapendwa kuvaliwa na watu maarufu na wasanii nyota duniani.

Kwa wasanii wa hapa nchini, Vanessa Mdee, ni mpenzi wa pete za aina hii. Mtu anavaa kuanzia chini ya vidole hadi juu.

Hata hivyo, kuna aina tofauti, lakini zenye vito vya kung'aa zinapendwa zaidi.

Jinsi za kuzivaa

Pete za vifundoni zinapendeza zaidi kama kucha zimetengenezwa vizuri.Unashauriwa kuzisafisha na kupaka rangi ili kuongeza mvuto.

Aina hii ya Pete zinafaa kuvaliwa mahali popote ikiwa ofisini, matembezi au sehemu za burudani.

Mwanamke ni urembo bwana, lazima uonyeshe unachotaka, si kwa maneno tu.

Aina

Kuna aina tofauti za knuckle rings, zipo kubwa lakini aina hizi zinauzwa zikiwa na ndogo, hapo ni wewe tu utakavyotaka kuzivaa.

Pia kuna pete moja moja, ambazo zinauzwa kwa seti lakini. kuna ambazo zipo kama pingu na ziko pamoja. Hizi pete hazivalishwi kwenye vidole vyote, lakini unashauriwa kuzilinganisha kwa rangi ili kuleta matokeo mazuri.







# MAPISHI

## Na Mary Geofrey

## KABABU ZA NYAMA

**Mahitaji**

MINOFU ya nyama ya ng'ombe, kuku au samaki, yai moja, kipande kimoja cha mkate, pilipili hoho moja, kitunguu maji kimoja, kitunguu saumu kimoja, karafuu iliyosagwa, chumvi na limao.

Namna ya kuandaa

Kitunguu maji na pilipili hoho, vyote vikatwe vipande vidogo, ponda kitunguu saumu kwenye kinu, halafu viweke pembeni.

Andaa nyama ya samaki, kuku au ya ng'ombe kwa kukata vipande, ioshe, kisha ichemshe na weka ndimu na chumvi.

Nyunyuzia pilipili manga, usiongeze maji kwenye nyama, acha ikauke halafu weka kitunguu.

Loweka kipande cha mkate kwenye maji, kitoe na kikamue kisha changanya na mayai yaliyopasuliwa na kukorogwa na kuchanyika vizuri.

Bandika kikaangio jikoni, weka mafuta mengi kiasi, subiri yachemke na tengeneza umbo la mviringo kutoka kwenye nyama, samaki au kuku, kisha chovya kwenye rojo la mkate na mayai.

Tumbukiza mviringo wa mchanganyiko kwenye mafuta, mmoja baada ya mwingine ili kupata matokeo mazuri kwa kutumia kijiko kikubwa chenye madundu ili kuchuja mafuta.

Mchanganyiko wako ukae kwenye mafuta kwa muda wa sekunde tano hadi nane mpaka uwe rangi ya kahawia na hapo utakuwa umeiva vizuri.

Ipua na acha vikauke na tayari msosi wako utakuwa tayari kwa kuliwa. Unaweza kula kama kifungua kichwa au wakati wowote kwa kutumia soda, juisi au maji.



# MAISHA NI NYUMBA

## Na Elizabeth Zaya

# HII NDIYO SEBULE INAYOITA



SEBULE kwa kawaida ni sehemu ya ndani ya nyumba ambayo ni maalumu kwa kupumzikia, kujumuika na kupokelea wageni.

Sebule siyo chumba cha kawaida tu, bali ni sehemu inayopaswa kuwa na sifa za kipekee kwa sababu ndiyo huonyesha ubora wa nyumba na aina ya watu wanaoishi humo.

Kutokana na umuhimu wa sebule, kuna haja ya kuzingatia mambo mbalimbali ikiwamo mpangilio wa vitu vinavyopaswa kukaa, vinavyovutia zaidi katika kupokea wageni, na muonekano wake wanapokuwa wanaingia.

Mpangilio huo wa sebule utategemea pia kiasi cha utulivu ambacho kinatakiwa kuwapo ili kisizalishe kelele za kuathiri shughuli nyingine katika nyumba ikiwamo za kujisomea.

Ni vyema sebule iwe inachangamsha, inaleta hamasa ya kukaribisha wageni, hamasa ya maongezi, iwe inaleta hali ya kupumzika. Isiwe inachosha, inaogopesha wala kuboa.

Mpangilio wa vitu na samani mbalimbali katika sebule unaleta ladha fulani. Ni muhimu kuchagua vitu vyenye kuleta ladha nzuri unayotaka katika sebule yako.

Pia kiasi cha vitu ambavyo ungependa viwapo sebuleni. Umbali kati ya kochi na kochi, luninga na vinginevyo huathiri ukubwa wa sebule yako hivyo unatakiwa kuwa makini katika kuvipangilia.

Zingatia rangi za vitu unavyoweka katika sebule yako, kwa kuhakikisha havipishani sana, epuka sebule kuwa na rangi nyingi zinazotokana na vitu vilivyomo humo kwa sababu zitachosha macho na hakutokuwa na utulivu wa nafsi.

# MPANGILIO

# DONDOO MUHIMU YA NAMNA YA KUWEKA KIFAA CHA KUWEKEA VISHUNGI VYA SIGARA SEBULENI


KIFAA cha kuwekea vishungi vya sigara ni muhimu kuweka sebuleni ili kuepuka hatari ya moto.

1: Weka kifaa chako cha kuzimia sigara juu ya meza ndogo.
2: Hakikisha kinakuwa kisafi kila wakati, pale kinapojaa jivu au vishungi ni lazima kutupa sehemu salama.
3: Usiruhusu kushikwa na watu hasa watoto wadogo, kila mara ufanyike ukaguzi kama kipo salama.
4: Kifaa hicho kiwe cha chuma au udongo mgumu ambao hauruhusu joto kupenya.





# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2020
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
Muda mfupi Umetoka Kuomba Ridhaa ya kuchaguliwa utuletee maendeleo, Je, kwa Mfano huu nani AKUCHAGUE?
Kujua Tabia Zangu Mapema Na Kuziweka MUBASHARA Ni sehemu ya KAMPENI
SHIKAMUU BABU. Eti ndio wewe Nimekuona kunako Tivii Umesema Usipopigiwa Kura UTAVURUMISHA VURUMAI?
WE' MTOTO ACHA KUNICHURIA MWENZAKO HADI UMRI HUU, JELA NAIONA KWA NJE!
SERA
Unaacha kunipigia NdogoNdogo kwa Wanawake wenzio ili nishinde ushindi wa Kishindo, Upo Bize na Vikoba! UNA AKILI KWELI?
Hata hao unaonituma Wakusapoti, Nao Pia wapo Bize na Vikoba... Nahisi nao hamnazo kama mimi WATAKUPIGIAJE?
'NIMEGHAILI' Nipo Taiti sana! Nitagombea Miaka ijayo nikiwa Hai
We sema NGOMA NZITO!
UTAWASIKIA, 'Mkinichagua maji ya MAFURIKO katikati ya JIJI yakiingia YATA-KAMATWA!
HA HA HA!
Nna Uhakika Mimi ni Mshindi Na Nikidhurumiwa NALIAMSHA DUDE MBELE YAKO...
Kama ushindi Unapatikanaga nje ya Boksi la KURA, basi siku hiyo JARIBU UONE!
*KINYUNYIZO CHA LEO... ...UKICHUNWA AKILI YA KUTAFUTA INAKUJA...

# Dhahabu yazidi kupungua duniani

**LONDON, Uingereza**

HOFU imetanda baada ya kiwango cha dhahabu duniani kuzidi kupungua na kubaki tani 50,000 pekee haijachimbwa.

Utafiti uliofanywa na wanajiolojia wa Marekeni, unaonyesha kila siku kiwango hicho kinazidi kushuka na kuleta tishio siku moja dunia itabaki tupu bila kuwepo kwa madini hayo yenye thamani kubwa.

Hata hivyo, katika tafiti zingine tofauti za miaka ya hivi karibuni, zimefichua uwepo wa dhahabu nje ya sayari ya dunia.

Kiwango hicho kikubwa cha dhahabu ambacho sio cha kawaida imewafanya wanasayansi kukuna vichwa kwa miaka kadhaa wakijaribu kutafuta wapi kinapatikana.

Ripoti iliyotolewa wiki hii, inaashiria idadi ya dhahabu iliyopo duniani ni kubwa kuliko ile iliyokadiriwa awali.

Ripoti hiyo iliyochapishwa katika jarida unajimu, ilisema chanzo kikuu cha dhahabu duniani kwa sasa ni mgongano wa nyota za aina ya neutroni na si rahisi kuelezea kiwango cha chuma kilichopo duniani na angani.

"Dhahabu na madini mazito hutengenezwa kutokana na nguvu nyingi zinazovyutana duniani. Hatahivyo michakato hii haitoshi kutoa dhahabu yote tunayoiona katika dunia, "alisema. Mtaalam wa nyota Chiaki Kobayashi, kutoka Chuo Kikuu cha Hertfordshire.

Kobayashi, alisema madhumuni ya utafiti huo ni kupata habari sahihi zaidi kuhusu asili halisi ya kile kinachoitwa chuma nzito. "Dhahabu ni sehemu ya mambo mengi katika maisha yetu,"alisema.

Asili hiyo ya utengenezaji wa dhahabu ndiyo inayokubalika kuwapo kwenye sayari ya Dunia. Kulingana na utafiti uliosimamiwa na Kobayashi, lazima kuwe na vyanzo vingine ambavyo vitazalisha dhahabu nyingi.

**BBC**



Raia wa Syria wakiwa katika lori wakivuka mpaka wa Kobani kuingia Uturuki wakati wa wimbi la wakimbizi likizidi kuendelea kukimbia vita Kaskazini Mashariki mwa Syria juzi **(PICHA: AFP)**

# Waziri ashtakiwa dawa za kulevya

**WASHINGTON, Marekani**

WAZIRI wa zamani wa ulinzi wa Mexico, amekamatwa na kufunguliwa mashtaka ya kujihusisha na biashara ya dawa ya kulevya na kutakatisha fedha nchini Marekani.

Salvador Cienfugos, aliyekuwa na nguvu katika uongozi wa Rais, Enrique Pena Nieto, kuanzia mwaka 2012 hadi 2018.

Waziri huyo alikamatwa juzi kwenye uwanja wa ndege wa Los Angeles, wakati akiwa kwenye safari ya kifamilia.

Hati za mashitaka zilizopatikana zinaonyesha kuwa, Salvador, anatuhumiwa kuzalisha na kusambaza maelfu ya kilo za cocaine, heroin, na bangi, nchini Marekani, kati ya Disemba 2015, na Februari 2017.

**DW**

# Waziri Mkuu New Zealand apata ushindi wa kishindo

**WILLINGTON, New Zealand**

WAZIRI Mkuu wa New Zealand, Jacinda Ardern, amepata ushindi mkubwa katika uchaguzi mkuu uliofanyika jana.

Ushindi huo unakipa chama chake cha Labour nafasi ya kuunda serikali bila ya kushirikisha vyama vingine.

Baada ya kuhesabu kura kufikia theluthi mbili, chama cha Labour kimepata asilimia 49.2 ya kura zote, huku kikitarajiwa kupata viti 64 katika bunge la New Zealand lenye viti 120. Ushindi huo ulielezwa kuwa wa kihistoria, kwani hakuna kiongozi mwingine aliyepata ushindi wa aina hiyo tangu nchi hiyo ilipoidhinisha mfumo wa uchaguzi unaozingatia uwiano wa uwakilishi mwaka 1996. Hata hivyo, kiongozi wa chama kikuu cha upinzani, Judith Collins, alimpigia simu Waziri Mkuu Ardern, akikubali kushindwa.

Chama cha kihafidhina cha National Party kinachoongozwa na Collins, kinatazamiwa kuambulia viti 35 vya wabunge, hayo yakiwa matokeo mabaya kwa chama hicho katika kipindi cha miaka 20.

**DW**

# Watu mil. 39 waambukizwa virusi corona

**BERLIN, Ujerumani**

MAAMBUKIZI ya virusi vya corona yamefikia watu milioni 39 duniani kote, kati ya yao milioni 1.1 wakipoteza maisha.

Kulingana na ripoti ya Chuo Kikuu cha John Hopkins, idadi hiyo ni hadi kufikia juzi jioni. Marekani inaongoza kwa kuwa na watu milioni nane, walioambukizwa maradhi ya COVID-19.

Taarifa hiyo ilisema Marekani imepoteza watu 218,000, kutokana na maradhi hayo hadi jana.

Nchi zinazofuata katika orodha hiyo ni India, ambako watu milioni 7.4 wameambukizwa na Brazil, milioni 5.1.

Katika visa vipya vya maambikizi, juzi pekee walithibitishwa watu 400,000 walioambukizwa, kwa mujibu wa takwimu zilizokusanywa na shirika la habari la AFP.

Katika bara la Ulaya, idadi ya maambukizi mapya yamevuka asilimia 44 kwa wiki moja, huku watu 121,000 wameambukizwa virusi hivyo.

Baadhi ya nchi za Ulaya zimeanza tena kuchukua hatua za kukabiliana na kasi ya kusambaa kwa virusi hivyo, ikiwamo kufungwa migahawa, maduka, na maeneo ya wazi.

Ujerumani kwa upande wake, imethibitisha watu wengine 7,830 walioambukizwa virusi hivyo ndani ya masaa 24.

**DW**

# Makombora yaua saba Azerbaijan

**BAKU, Azerbaijan**

WATU saba wameuawa baada ya kombora kuangukia kwenye nyumba za raia katika mji wa Ganja nchini Azerbaijan.

Mashambulizi hayo yalifanyika saa chache, baada ya kushambuliwa kwa mji mkuu wa jimbo la Nagorno-Karabakh, Stepanakert, ambao ni kitovu cha vita kati ya Armenia na Azerbaijan.

Waandishi wa shirika la habari la AFP mjini Ganja, wameripoti kushuhudia nyumba zikigeuzwa vifusi, huku watu wakikimbia ovyo kunusuru maisha yao.

Wafanyakazi wa huduma za uokozi, waliendelea kusaka majeruhi.

Msaidizi maalum wa Rais wa Azerbaijan, Ilham Aliyev, alisema zaidi ya nyumba 20 ziliharibiwa katika mashambulizi hayo,

Alisema watu wengine 10 waliuawa kwenye mji huo huo, kutokana na makombora.

Uturuki na Urusi, ambazo zinaunga mkono pande tafauti za mzozo huo, zimetoa wito wa kusitishwa mapigano.

**DW**

## MAKALA

# Miaka 21 bila Mwalimu je, tuko wapi?



Na Magabilo Masambu

KILA ifikapo 14, Oktoba ya kila mwaka Tanzania tumekuwa na siku ya maadhimisho ya kumkumbuka Baba na mwasisi wa Taifa letu Mwl. J.K. Nyerere, kama siku muhimu ya kutafakari mahali tulipo sasa, alipotuacha na tunakoelekea.

Bila shaka ni wajibu wa kila Mtanzania kujiuliza tuko wapi sasa tangu mzee wetu atutoke? Mwalimu anakumbukwa kwa mengi ndani ya nchi yetu, Afrika na pengine duniani kwa wale waliopata kumsikia. Alifanya mengi nitataja machache kisha tujitazame wapi tulipo na je, tuendelee hivi hivi au tubadilishe uelekeo ili turudi tulikotoka kwa manufaa ya tunakoelekea?

Jambo mojawapo tunaloweza kujivuna na kila wakati litufanye tumkumbuke ni juu ya umoja wetu, kuna baadhi ya watu hudhani kwamba Tanzania ilijikuta tu ni wamoja, tunafahamu kuwa tuko zaidi ya makabila 120, tunazo dini zetu mbalimbali, tuna watu wenye rangi mbalimbali, lakini bado tumedumu kama ndugu kwa muda mrefu zaidi.

Tukiachana na baadhi ya mbwembwe za wanasiasa naweza kukiri kabisa kwa dhati kuwa sisi bado ni wamoja na hasa wananchi wa kawaida bado tunapopata matatizo tunasaidiana kama kaka na dada, Watanzania bado tuna upendo ambao wengi barani Afrika hawana, kuna wakati huwa nafikiri kwamba inawezekana Tanzania ndiyo nchi yenye watu wema, wenye roho za huruma kuliko wenzetu wengi na hasa ukanda huu wa Afrika, maana kwa tunayoyasikia mahali kwingine ni ya kusikitisha japo yameanza pia kutokea hapa kwetu!

Mnamo Machi 13, 1995 kuelekea uchaguzi mkuu wa kwanza wa mfumo wa vyama vingi uliofanyika Oktoba 1995, Mwalimu alizungumzia habari za nyufa katika taifa letu.

Alitaja nyufa hizo alipofanya mkutano na Klabu ya Waandishi wa Habari wa Tanzania katika hoteli ya Kilimanjaro. Akasema "Nchi changa ni sawa na nyumba mpya, unapojenga nyumba mpya unaifurahia, lakini unapotokea mtikisiko utawaonyesheni sehemu mbovu za nyumba ile."

Akasema anaziona nyufa katika paa, kuta, lakini pia katika msingi. Akataja nyufa tano ambazo ni Muungano, Kupuuza na kutojali Katiba ya nchi, Kuendesha mambo bila kujali Sheria, Rushwa na tano akasema Ukabila na Udini.

Leo ni miaka 21 hatunaye je, katika hizi nyufa tano tumekwenda mbele ama tumerudi nyuma kiasi gani? Je, tunao mwelekeo mbaya au mzuri? Tunamuenzi ama hatumuenzi katika maeneo hayo? Je, watu wameacha kujihalalisha kwa udini, ukabila, ukanda au aina nyingine yoyote inayofanana na hayo? Haya ni maswali tunayopaswa kujiuliza kama Watanzania wa leo na kesho.

Sitaki kuamini kwamba tumeshakuwa na hali mbaya sana katika maeneo yote hayo, nafikiri kama kuna maeneo yanalalamikiwa lazima hatua za makusudi zichukuliwe ili kuziba nyufa hizo zisibomowe nyumba kwani ikibomoka wote tutalala nje.

Eneo lingine ni juu ya viongozi kujilimbikizia mali, sasa hivi tuna mchakato wa uchaguzi kampeni zinaendelea, hatujasikia mgombea yeyote wa nafasi yoyote akisema kwenye jukwaa kwamba anaomba kazi hiyo ili akawe tajiri, wote wanasema nichaguweni niwaletee maendeleo, nisimamie haki zenu, nitawafanyia hivi na vile na mambo mengi ya sampuli hiyo, nachoshindwa kuelewa ni kwamba akili za namna hii huwa zinakwenda wapi tukishapata madaraka? Mwalimu aliishi alichohubiri na wanasiasa wengi wamebaki tu kutumia jina lake kujihalalisha bila kuyaishi matendo yake. Tuyaishi na tutende tunachohubiri.

Mwaka 2016 nilipata nafasi ya kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Taasisi ya Mwl. J.K.Nyerere, ndugu Joseph Butiku, aliniambia sifa kubwa aliyokuwa nayo Mwalimu ni kusikiliza hata kama jambo unaloongea litaonekana kwa wengine si la maana, lakini alisikiliza bila kuchoka. Sifa ya kiongozi bora ni kuwa na uwezo mkubwa wa kusikiliza kila mtu bila kujali tofauti zake ama itikadi ya chama, dini yake, kabila lake, umbo lake mrefu au mfupi ilimradi ana jambo la kusema basi ni muhimu kusikiliza kwasababu kujifunza hakuna mwisho na katikati ya ujinga huwa kuna akili.

Leo kiongozi anaomba kura kwa unyenyekevu akishapata anatoa na maelekezo kwa katibu wake wakija waambie sipo tabia gani hizi kama hutaki kero za wananchi usigombee.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Arusha-Tanzania**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Black Moses, Kokoliko walivyotamba kwenye disko



Na Adam Fungamwango

MWISHONI na mwanzoni mwa miaka wa 1990 kulitokea mapinduzi makubwa ya muziki nchini Tanzania hasa kwa upande wa disko.

Si kwamba muziki huo haukuwapo zamani, la hasha, bali ulikuwapo tangu enzi za kumbi za Mbowe Hotels, YMCA, Rungwe Oceanic, Silver Sands, Msasani Club, Washirika (maarufu kama Maggot), Motel Villa de Tanzanie, UFI Club na nyinginezo nyingi.

Hiyo ilikuwa kwa Dar as Salaam, kwa Tanga ilikuwa Mkonge Hotel na Limachia na kule Tabora kulikuwa na Rufita, Mwana Isungu Honey Pot, Tabora Hotel, Muungano Mess na vyuo vya Nyuki na Uhazili.

Iringa kulikuwa na Ruaha International na Mafinga ambako Super Kimbe Disco Sound iliwika sana, watu walikuwa wakijimwayamwaya katika kumbi za Magereza na John's Corner. Hiyo ni kwa uchache lakini kila mkoa kulikuwa na kumbi maarufu za dosco au muziki wa dansi. Pamoja na kumbi hizo, mwishoni mwa miaka ya 1980, kulitokea mabadiliko au mapinduzi makubwa ya muziki huo kwani walitokea baadhi ya watu waliokuwa hodari katika kucheza muziki ule wa Ulaya na Amerika, maarufu kama 'debe' wakiwaigiza wanamuziki maarufu kama Michael Jackson. Pia walitokea wale walioiga kucheza muziki wa Congo wakati huo ikiitwa Zaire. Miongoni mwa watu hao ni Athuman Digagida, Super Ngedere na Mussa Simba, maarufu kama Black Moses. Kwa upande wa muziki wa Kizaire, alikuwapo Shadrack Athuman Guga, maarufu kama Kokoliko ambaye mashabiki wake walimpachika jina la Bileku Mpasi wa Tanzania.

Na hii ilisababishwa na televisheni kuanza kuingia nchini. Zilipoanza kuingia nchini, japo zilikuwa chache, baadhi ya vijana walianza kupata bahati ya kuwatazama wanamuziki maarufu wa nje. Vijana wengi wakajifunza mitindo mbalimbali ya uchezaji wa muziki huo na kuwa mahiri kiasi cha kuanza wengine kujiamini na kuanza kufanya kazi ya kuburudisha watu kwenye kumbi mbalimbali za burudani. Hii ilivutia wengi na kuanza kuwakodi kwenye sherehe mbalimbali za harusi, hafla ya kiserikali na nyinginezo.

Ikaenda mbali zaidi kikaundwa mpaka Chama cha Muziki wa Disko Tanzania (TDMA) ambacho kilianza kuandaa matamasha na mashindano ya disco ambayo yalitokea kuwa maarufu na kuwafanya vijana hao mbali na kuishi kwa kipato cha kucheza muziki huo pia kuwa maarufu. Mitindo iliyokuwa ikichezwa na kupendwa kwa wakati huo ya kizungu ni Pop, ambayo mfalme wake alikuwa Michael Jackson. Sina haja sana ya kuelezea staili hii kwani wengi wanajua uchezaji wa Michael.

Staili nyingine ni 'break dance.' Hii ni staili ngumu ambayo mchezaji ni lazima awe na ufiti wa viungo, vinavyoweza kunyumbulika na kuweza kujipinduapindua kama mcheza sarakasi. Hii watoto wa mjini waliita 'mabreka'.

Halafu kuna 'funk' ambayo vijana wakati ule waliita 'mafanki', ni staili ambayo viungo kama mikono, mabega na vitu vingine tu hufanya kazi yake. Kulikuwa na 'heavy funk' na 'slow funk'. Kwa upande wa staili za muziki wa Congo, kulikuwa na mitindo ya 'Kwasakwasa', 'Tshamukwale' na 'Nzawisa'.

Miaka hiyo, wanamuziki kama Pepe Kale na kundi lake la Empire Bakuba walikuwa wakizuru sana nchini Tanzania na ndiyo miaka ambayo walitunga nyimbo kama 'Yanga Afrika' wakiisifia timu ya Yanga na walipokuja baadaye na kuondoka wakatunga wimbo wa 'Hidaya'. Lakini pia upo wimbo mwingine ambao haukupata maarufu sana lakini ulikuwa ni baada ya ziara yao nchini ukitungwa na kuimbwa na Papy Tex kwa lugha ya kiswahili 'Mpenzi Bupe'.

Miaka hiyo hiyo ya 1990, ndipo mwanamuziki Kanda Bongoman alipozuru nchini na kufanya onyesho kwenye Hoteli ya Kilimanjaro jijini Dar es Salaama, kiingilio kikiwa Sh. 100,000 za Kitanzania. Kiingilio hicho kilikuwa kikubwa kwa miaka hiyo lakini umati ulijaa kiasi kwamba kuna watu walizuiwa kuingia wakiwa na pesa zao mkononi. Sidhani kama kuna mwanamuziki wa Tanzania kwa sasa anayeweza kuweka kiingilio hicho akajaza watu kiasi kile.

Kama nilivyosema awali, Black Moses alikuwa mmoja wa wacheza disco wa viwango vya juu aliyepata kutokea Tanzania. Kwake kutwaa ubingwa wa taifa halikuwa jambo kubwa. Alikuwa na uwezo mkubwa wa kucheza miziki wenyewe wanaiita wa kizungu, 'funk', 'pop' na 'break dance'.

Black Moses ambaye ni marehemu, kulikuwa kunawaka moto kama mpinzani wake akiwa Bosco Cool J. Ilikuwa hatari sana kwenye kumbi za Vijana Social Hall, Kwa Macheni, Lang'ata Social Club na Bahama Mama.

Kuna kijana mmoja kutokea Mwanza aliitwa John Maganga. Ni mcheza disco aliyejitengeneza na kufanana kabisa na Michael Jackson kiasi cha kushangaza wengi. Aliitwa Michael Jackson wa Tanzania. Wajihi wake, nguo, na hata alivyojitengeneza mwenyewe ilikuwa kama unakutana naye unaweza kusema Michael. Kwa kiasi kikubwa alizitendea sana haki nyimbo za Michael kwenye uchezaji na kusababisha asiwe na mpinzani kwenye eneo hilo.

Unamkumbuka Prince Max, yule aliyekuwa mwigizaji ambaye wajihi wake kwa sasa unafanana sana na mwigizaji wa sasa Mkwere? Pamoja na uigizaji, pia alikuwa mahiri kwenye kusakata disco na mara nyingi anga zake zilikuwa kwa Macheni.

Disco lilipambwa sana na wasanii kama Athumani Digadiga, Dogodogo Kadoda, Super Ngedere, King Jobiso, Small Jobiso na wengineo.

Kuna jamaa mmoja anaitwa Cadet Bongoman. Huyu alijipambanua na kujitengeneza kama Kanda Bongoman, akivaa mapama na nguo kama mwenyewe, huku akiwa ni mtaalam wa kucheza nyimbo zake tu.

Kama vile haitoshi kulikuwa na mtu mmoja aliyeitwa Kokoliko. Alikuwa na uwezo mkubwa wa kucheza nyimbo za Kicongo wakati huo Zaire na hasa za Empire Bakuba ya Pepe Kalle. Kwa wajihi, alifanana sana na Bileku, rapa ambaye jina lake halisi lilikuwa Djuna Mumbafu. Kokoliko alikuwa akipenda kuvaa nguo kama Bileku, na hata bendi ya Empire Bakuba ilipokuwa ikifanya maonyesho yake nchini ilikuwa ikisafiri naye mikoani na kucheza pamoja na Bileku, kiasi cha kuonekana kama Kulwa na Dotto.

Msanii huyo alikuwa akimpelekesha vilivyo Bileku kiasi cha mwenyewe kumkubali mpaka kumuachia zawadi mbalimbali anapoondoka. Wasanii hao na muziki wao wa disco walidumu kwa muongo mmoja, hadi mwanzoni mwa miaka ya 2000 walipoanza kuzimwa na mambo mawili. Moja utandawazi ambapo watu wengi sasa walianza kumudu kumiliki televisheni majumbani, hivyo kuwa na uwezo wa kutazama wakiwa majumbani na taratibu maonyesho na kusababisha watu kupungua. Mwanzoni mwaka 2000 kulianza mapinduzi mengine ya muziki wa dansi wa Kitanzania wenye vionjo vya Congo kama Diamond Sound, FM Academia, Acudo Sound, Mokibo Sound, African Stars 'Twanga Pepeta', bendi ambazo zilikuwa zikipiga muziki kuiga mapigo ya bendi za Wenge Musica, Extra Musica, Koffi Olomide, Defao na kuimba kwa kiswahili.


Muziki wa aina hii ulichengua mashabiki wengi wa muziki na hata baadhi ya wacheza disco hasa wa kike walijiunga na bendi hizo kabla ya kuingia kwa muziki wa kizazi kipya miaka ya 2000.

# HADITHI

WASWAHILI wanasema mshika mawili moja humponyoka na karamu mbili zilimshinda fisi. Cecilia, msichana mwenye kila sifa ya kuitwa mrembo, anaangukia kwenye mapenzi ya vijana wawili. Mmoja ni fukara na mwingine mwenye uwezo. Kutokana na mwenyewe Cecilia kutokuwa na msimamo wenye kueleweka, anawaingiza vijana hao kwenye chuki na visasi, vilivyoambatana na wivu uliopindukia na kusababisha maafa makubwa. Ni kisa cha kusikitisha, kutisha na kuhuzunisha, lakini chenye elimu kubwa.

# Adui Namba Moja-4

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**




CECY alijua kuwa ana mpenzi aitwaye Mashaka, lakini hakuonekana kuwa na msimamo.

Awali alisita. Lakini zawadi za magauni, blauzi, vipedo, vitenge, pesa vilimlainisha moyo.

Taratibu alianza kumsaliti Mashaka. Akawa na wapenzi wawili kwa wakati mmoja.

Siku zote penzi haligawanyiki. Haiwezekani ukawa na mpenzi zaidi ya mmoja, likaganyika nusu kwa nusu.

Hata ukiwa na wake wanne, ni lazima penzi litaelemea kwa mmoja zaidi.

Wazee wa zamani walisema dunia, mali na shamba vyote vinagawanyika, lakini siyo penzi. Lenyewe litafanya kila njia, upande mmoja litazidi.

Ndivyo ilivyokuwa. Kutokana na kupofushwa na uwezo wa kipesa wa Zahir, penzi likaelemea zaidi kwake kuliko kwa Mashaka.

Na kibaya zaidi aliona kama vile anamletea kiwingu, hivyo alitaka kuwa huru na mpenzi wake Zahir. Watanue. Waende popote pale bila kuhofia chochote wala vikwazo. Hivyo ndivyo Cecy alipoamua kumtema Mashaka.

Hata hivyo kwa mbali kama kuna kitu asichokijua kilikuwa kikimwambia kuwa alikuwa anafanya kosa kubwa.

Kwanza alikuwa akimkatili mtu anayempenda kwenda kwa mwanamume ambaye haijulikana kama anampenda au kumtamani.

Hakurudi nyuma. Kichwa chake kilishashikilia msimamo huo, akaamua kubaki wa msimamo wake.

************************

Ni miezi miwili ilipita. Mapenzi ya Cecilia na Zahir yaliendelea. Yalikuwa mapenzi ya nipe nikupe. Siku Zahir akimhitaji Cecy anamtafuta kwenye simu wanakutana sehemu na kumalizana.

Cecy hakuwahi kupelekwa nyumbani kwa Zahir.

"Kwani wewe umeoa?"

"Kwa nini ?"

"Mbona kila siku nakwambia nipeleke nyumbani kwako unakataa?" Alilalamika Cecy.

"Hapana ila naishi na ndugu zangu, sasa haiwezekani nikupeleke wewe pale."

"Hadi lini?"

"Labda nikikuoa. Unajua sisi kwetu watu wa dini sana, hawawezi kukubali nifike pale na mwanamke tu ambaye sijamuoa. Nyumba ni yangu, lakini linapokuja suala la familia tena, hakuna mambo ya hapa kwangu." Alisisitiza huku akikwepesha macho yake na yasitazamane na ya Cecy.

"Umesema labda."

"Ndiyo."

"Ina maana kuwa unaweza kumuoa mwingine?"

"Sina maana hiyo Cecy."

"Wee wee, usinipotezee muda Zahir. Kama hutaki kunioa uniambie mapema nijue ustaarabu mwingine."

Ni kweli Cecy alikuwa akipata kila kitu alichotaka kutoka kwa Zahir.

Akiwa na shida ya pesa, nguo, kwenda kwenye starehe, na vingine vinavyofanana na hivyo wala hakuwa na tatizo.

Alichokimisi yeye ni mapenzi. Mapenzi yenyewe halisi. Kiasili mapenzi si pesa. Pesa imekuta mapenzi duniani. Pesa inachofanya ni kuboresha mapenzi tu. Mapenzi yanaanza pesa baadaye. Hakuna sehemu ambayo inaanza pesa halafu yakaja mapenzi.

Mapenzi ndiyo kitu pekee kinachoweza kumtoa binadamu Oysterbay, Mikocheni, Mbezi Beach kwenye nyumba ya kifahari akaenda kuishi kwenye nyumba ya mbavu za mbwa Manzese au Mburahati.

Hayo hayo mapenzi, yanaweza kumtoa mtu na akili zake kwenye kitanda cha futi sita kwa sita na kwenda kulala kwenye kitanda cha telemka tukaze tena chenye kunguni na asiweze kabisa kuona adha yake, bali kufurahia maisha.

Cecy, pamoja na pesa alizokuwa akihongwa na Zahir, bado alimisi mapenzi. Alimisi kushikwa mkono na kutembea na mpenzi wake barabarani watu wakiwaangalia.

Kushikiwa pochi, au kibegi chake pale anapohitaji kufanyiwa hivyo. Kununuliwa zawadi ndogo ndogo tena bila kuomba. Pia alimisi kusifiwa uzuri na urembo aliojaaliwa na mwenyezi Mungu, kupewa maneno ya faraja na upendo kiasi cha kuwa na amani ya moyo.

Kadhalika alikosa kuliwazwa nyakazi zote za shida na raha. Kikubwa kuliko vyote ni maneno ya utani na vichekesho ambavyo vilikuwa vikimfanya avunjike mbavu.

Haya yote yalifanywa na Mashaka. Kwa sasa Mashaka amempiga chini. Pamoja na ufukara wa Mashaka, aliona utofauti.

Kwa Mashaka, Cecy alikuwa mwanamke. Mwenye haki ya kupendwa, kupewa moyo, kulindwa na kudekezwa.

Kwa Zahir, Cecy alijiona kama ni kifaa cha matumizi tu. Hakuwa akiambiwa kitu chochote zaidi ya kupigiwa simu "Uko wapi?", "Tukutane baa."

Mara ya mwisho kuambiwa amependeza ilikuwa ni siku ya kwanza alipopewa lifti na kutongozwa na Zahir.

Siku zote alionekana ni mwanamke wa kawaida tu. Hawajawahi kukaa na mpenzi wake huyo mpya na kuongea maneno ya maana au ya utani na mzaha, badala yake ni kwenda kwenye kumbi za starehe na kulala kwenye mahoteli makubwa, baada ya hapo wanaachana.

> **"Cecy, kumbuka kuwa uko na mtu sahihi anayekuthamini na kukupenda kwa dhati. Najiona mwenye bahati kuwa nawe. Wewe ni zawadi yangu niliyopewa." Akakumbuka pia maneno matamu aliyokuwa akipewa na Mashaka enzi za penzi lao.**

Kwa mbali alianza kumkumbuka Mashaka, ingawa alijilazimisha asifanye hivyo.

Alikumbuka upendo wa mwanamume huyo ambaye miezi mingi iliyopita alimtolea maneno ya kashfa hospitalini mama yake alipolazwa.

Kama haitoshi akaishia kumwambia asimfuatefuate tena.

Na kweli hadi leo hii hajapata hata meseji kutoka kwa Mashaka, achilia mbali simu.

"Usijali mama, tutakuwa pamoja kwa shida na raha, tutaambatana na kubembelezana kama vipepeo wawili wapendezao." Anakumbuka moja ya meseji ambazo alishawahi kutumiwa na Mashaka.

"Cecy, kumbuka kuwa uko na mtu sahihi anayekuthamini na kukupenda kwa dhati. Najiona mwenye bahati kuwa nawe. Wewe ni zawadi yangu niliyopewa." Akakumbuka pia maneno matamu aliyokuwa akipewa na Mashaka enzi za penzi lao.

Alimisi aina hiyo ya upendo. Badala yake sasa meseji zinazominika na simu ni la kumlazimisha aende anapoambiwa atamkuta, au kuja kuchukuliwa na gari. Lakini pia lawama nyingi kama vile "Mbona hupokei simu?" "Uko na mabwana zako ee?", "Mbona hapo unapoongea kuna makelele sana, uko baa nini?"

Yalikuwa maisha ya mapenzi mapya wa Cecy ambayo hakuyazoea.

"Maji yameshamwagika, hayazoleki." Alijisemea mwenyewe.

***************************

INAENDELEA JUMAPILI

## Steve Nyerere ampongeza Kiba



MSANII wa filamu za Bongo Muvi, Steve Nyerere, amempongeza, mwanamuziki Ali Kiba kwa kuonyesha moyo wa kuwathamini waigizaji.

Steve amesema hayo baada ya tukio la Kiba kuwaombea bajeti kwa Rais Dk. John Magufuli, kwa ajili ya kutengenezwa filamu ya Baba wa Taifa, Mwl Julius Nyerere.

Amesema kauli yake imetoka kwa mtu makini na ndio maana anaitwa Mfalme na alichokifanya kinaendana na heshima yake.

# SHAMSA

## ana mazito kwa wanaomfuatilia



MWIGIZAJI mkongwe wa filamu nchini, Shamsa Ford, ameamua kuandika ujumbe mzito kwa baadhi ya watu wanaopenda kuwahukumu kwa matendo yao.

Katika ujumbe aliouweka katika ukurasa wake wa Instagram, Shamsa, amesema wao kama mastaa ni binadamu ambao wanapitia matatizo kama watu wengine.

"Wengine wakituona kwenye mitandao wanatuhukumu tofauti, sisi ni binadamu kama nyie, wakati mwingine tunapitiwa kama binadamu wengine kwa sababu hakuna aliyekamilika zaidi ya Mungu. Maisha yetu pia huwa tunaishi kwa kumtegemea Mwenyezi Mungu, tusijisahau sana na dunia"

Kisha meendelea "Kulikuwa na matajiri wengi, wazuri wengi, watu maarufu wengi leo hii hatupo nao duniani, tuishi kwa kuthaminiana epuka kumuumiza mwanadamu mwenzio kwa makusudi sisi sote si chochote mbele ya Mwenyezi Mungu" ameongeza



## Ibraah Tz yamkuta ya bosi wake

TATIZO linalompata kila mara kiongozi wa lebo ya Konde Gang, Harmonize, kuondolewa na kurudishwa nyimbo zake katika mtandao wa You Tube, sasa limehamia kwa mwanamuziki wake Ibraah Tz.

Akaunti ya Ibraah Tz ya YouTube, ambayo umepakiwa nyimbo zake kadhaa sasa haipatikani na inaonyesha imefungiwa.

Kutokana na tatizo hilo, mashabiki wake wamekuwa roho juu kujua nini kimetokea, lakini bado huongozi wa Konde Gang hajatokea kuzungumzia tatizo hilo.

## HABARI MICHEZO



# ERIKSEN
## ATAPATA NAFASI YA KUCHEZA ZAIDI - CONTE

**MILAN, Italia**

ANTONIO Conte amesisitiza Christian Eriksen anaweza kupata nafasi yake hapo Inter Milan msimu huu.

Eriksen mwenye umri wa miaka 28, alijiunga na miamba hao wa Serie A kutoka Tottenham Januari, lakini amekuwa na wakati mgumu tangu kutua kwake pale.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark alisema wiki iliyopita kuwa anataka nafasi zaidi, akiwa ameanza katika mechi tisa tu za Serie A tangu ajiunge na Inter.

Wakati Conte alisema Eriksen alipewa nafasi yake, anatarajia nafasi zadi kwa nyota huyo wa zamani wa Ajax.

"Anacheza. Bila shaka nafanya chaguo la wachezaji kwa manufaa ya timu, naweza pia kukosea," alisema kocha huyo wa Inter akiwaambia waandishi wa habari.

"Hata hivyo, nina furaha kwa kile ambacho Eriksen anaipa Inter kwa sasa, nafikiri ana furaha kubwa na kundi la timu hii.

"Tutampa nafasi zaidi kwa sababu nina uhakika msimu huu utakuwa mgumu na mrefu."

# GUARDIOLA: BERNARDO ATAWIKA MSIMU HUU

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola anaamini Bernardo Silva atafurahia msimu mzuri kwa Manchester City baada ya kuwa na wakati mgumu msimu wa 2019-20.

Silva aliifungia Ureno dhidi ya Sweden kwenye mchezo wa Ligi ya Mataifa ya Uefa Jumatano, na alisifiwa na Guardiola.

Wakati msimu uliopita alihusika katika mabao 13 kwenye Ligi Kuu England - ikilinganishwa na yale 14 kwenye msimu wa 2018-19 - alitengeneza nafasi ndogo.

Silva alitengeneza nafasi 71, zikiwamo pasi za mwisho, msimu wa 2018-19 na namba hiyo ilishuka hadi 51 msimu uliopita, wakati alipocheza kwa dakika 824.

Guardiola alisema nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 alikuwa amechoka msimu uliopita, akiwa ameisaidia City katika ushindi wa mataji manne.

"Kuna wakati alikuwa majeruhi na hakufikia kiwango cha msimu uliopita, lakini hua inatokea," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Naamini msimu huu atakuwa kwenye kiwango bora, nina uhakika na hilo kwani naamini atakuwa na nafasi nzuri zaidi."




# Pogba akaribia kusaini mkataba mpya United

**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba anakaribia kukubali kuongeza mkataba mpya wa mwaka mmoja hadi mwishoni mwa msimu wa 2022.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa mwenye umri wa miaka 27 atakuwa nje ya mkataba mwishoni mwa msimu huu.

**Pogba ameanza mechi zote tatu za Manchester United za msimu huu, alikuwa pia sehemu ya kikosi wakati Manchester United ikiadhibiwa na Tottenham Hotspur kwa mabao 6-1 pale Old Trafford.**

Wakati wa mapumziko wa timu za taifa, Pogba alisema kujiunga na miamba ya soka la Hispania, Real Madrid ni ndoto ya kila mmoja.

Inafahamika kuwa makubaliano ya mkataba mpya kwa Paul Pogba yalifikiwa wiki kadhaa nyuma.

Pogba alijiunga na United kutokea Juventus kwa dau la pauni milioni 89 mwaka 2016.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR ATAKUWA FITI KUIKABILI MAN UNITED

Kocha wake asisitiza hana tatizo lolote baada ya kumpa mapumziko aliporejea kutoka kwenye...

**PARIS, UFARANSA**

KOCHA Thomas Tuchel amesisitiza Neymar atakuwa tayari kuivaa Manchester United baada ya nyota huyo wa Paris Saint-Germain kupumzishwa kwenye mchezo dhidi ya Nimes.

Neymar aliachwa katika kikosi cha PSG kilichoibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Nimes huku Kylian Mbappe akifunga mara mbili kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu Ufaransa uliochezwa juzi Ijumaa.

Mchezo huo wa Ligue 1 ulikuja siku tatu baada ya Neymar kufunga mabao matatu 'hat-trick' dhidi ya Peru kwenye mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia mjini Lima na kuipiku rekodi ya Ronaldo na kupanda hadi nafasi ya pili kwa wafungaji bora wa Brazil.

Tuchel alisema aliamua kumpumzisha fowadi huyo, lakini anatarajia Neymar kurudi kikosini wakati PSG watakapoanza mchezo wao wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumanne dhidi ya Manchester United.

"Ney hana tatizo lolote. Tulizungumza pamoja, kama nilivyofanya kwa Kylian," alisema kocha huyo wa PSG.

"Tulikuwa na majadiliano na niliamua kumpumzisha. Lakini atarudi kikosini tayari kuivaa Manchester United.

"Atakuwa uwanjani kwa uhakika kabisa."

PSG imekuwa bila Neymar katika mechi nne kati ya saba za Ligi Kuu msimu huu, akishinda tatu.

Wamekuwa na wastani wa mabao mawili katika kila mchezo bila yeye.

## KWA UFUPI

**ARTETA AMTEGA OZIL**
KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amemwambia Mesut Ozil kuwa ana miezi miwili ya kudhihirisha uwezo wake klabuni hapo, kiungo huyo hajacheza mechi yoyote ndani ya uzi wa Arsenal tangu Machi 7.**(Sky Sport)**

**FERNANDES AGOMBEWA**
BARCELONA na Real Madrid zimeonyesha nia ya kumhitaji kiungo mshambuliaji wa Manchester United na Ureno, Bruno Fernandes mwenye umri wa miaka 26.**(AS)**

**WATFORD YAIBANIA PALACE**
KLABU ya Watford inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza imekataa kumwachia winga wa Senegal, Ismaila Sarr mwenye umri wa miaka 22 kwenda Crystal Palace. **(Mail)**

**NYOTA BARCA WAGOMA**
WACHEZAJI wa Barcelona wamekataa kukatwa mishahara yao, ombi hilo lilipelekwa na Rais wa klabu hiyo, Josep Maria Bartomeu.**(BBC Sport)**

**RODGERS AMTAKA SLIMANI**
KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers amesema mshambuliaji wake, Islam Slimani mwenye umri wa miaka 32, bado yuko kwenye mipango yake licha ya kutokucheza kwa mchezaji huyo raia wa Algeria tangu mwaka 2018.**(Sky Sport)**

**KEANE KUINOA GALAXY**
MSHAMBULIAJI wa zamani wa Timu ya Taifa ya Ireland, Robbie Keane, ambaye ana umri wa miaka 40, ataelekea nchini Marekani kwenda kukinoa kikosi cha LA Galaxy. **(Mail)**

**AARONS ACHELEWA**
WINGA wa Newcastle United, Rolando Aarons amekwama kujiunga na Huddersfield Town baada ya mchezo huyo mwenye umri wa miaka 24 kushindwa kukamilisha taratibu za uhamisho kwa wakati. **(Shields Gazette)**

**SALIBA AITAMANI ETIENNE**
KOCHA wa St. Etienne, Claude Puel amesema mlinzi wa Arsenal mwenye umri wa miaka 19, William Saliba alikuwa tayari kurudi klabuni hapo kucheza kwa mkopo kabla ya dili kushindikana. **(L'Equipe, via Mail)**

**MC MANUS AMVUTA BABA**
BEKI wa timu ya wanawake ya Manchester United, Abbie McManus (27), amesema baba yake ambaye shabiki wake mkubwa ameamua kuachana na mahasimu wao, Manchester City na kujiunga rasmi na United. **(Sun)**

**BENRAHMA ATUA WEST**
WEST Ham imemsajili winga wa Timu ya Taifa ya Algeria, Said Benrahma akitokea Brentford kwa dau linalokaribia pauni milioni 30. Benrahma (25), amejiunga na timu hiyo kwa mkopo wenye thamani ya pauni milioni tano lakini baadaye anaweza kusaini mkataba wa kudumu wa pauni milioni 20 na kupewa bonasi ya pauni milioni tano. **(Mail)**

**RADEBE AIBEBA LEEDS**
BEKI mkongwe wa Leeds United, Lucas Radebe, anaitabiria klabu yake ya zamani iliyorejea kwenye Ligi Kuu England itafuzu kushiriki mashindano ya Ulaya ikiwa chini ya Marcelo Bielsa. **(Mail)**



HABARI MICHEZO

# AZAM YAPITA NJIA ZA YANGA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

MABAO matatu yaliyofungwa na wachezaji wa wawili wa kigeni Mzimbabwe Prince Dube na Mzambia Obrey Chirwa, yameifanya Azam kuendelea kubebwa na nyota wake wa kigeni mpaka sasa.

Dube alifunga mabao mawili juzi usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex dhidi ya Mwadui, bao moja likifungwa na Chirwa na kuipa timu hiyo ushindi wa mabao 3-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa kwenye raundi ya sita.

Azam ambayo mpaka sasa imeshafikisha mabao 12, yote yamefungwa na wachezaji wa kigeni na kuifanya timu hiyo kuongoza kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 18, ikishinda mechi zote sita ambazo imecheza, ikiruhsu mabao mawili tu.

Dube ambaye kwa sasa amekuwa gumzo kwenye Ligi Kuu msimu huu, ameifungia Azam mabao sita lakini pia akiongoza kwenye orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu, huku Chirwa akiwa amepachika mabao manne.

Wachezaji hao wawili, wameifungia timu hiyo jumla ya mabao 10, huku mawili yaliyobaki yakitiwa wavuni na Richard Djodi mchezaji kutoka nchini Ivory Coast na Ally Niyonzima ambaye ni Mnyarwanda.

Yanga ni timu nyingine kwenye Ligi Kuu ambayo magoli yao yote yamefungwa na wachezaji wa kigeni.

Timu hiyo ina mabao saba, ambayo yamefungwa na Lamine Moro (mawili) , Michael Sarpong ambao wanatoka Ghana akifunga bao moja.

Wengine ni Carlos Carlinhos ambaye ni Muangola, Haruna Niyonzima (Rwanda), Yacouba Songne (Burkinafaso) na Mukoko Tonombe ambaye ni Mkongomani.

Timu za Simba na Namungo, pamoja na magoli yao mengi kufungwa na wageni, Wabongo wamefunga pia.

Simba yenye mabao 14, yaliyofungwa na Meddie Kagere, Clatous Chama, Chriss Mugalu, Luis Miquissone, lakini mabao mawili kati ya hayo yamefungwa na Mzamiru Yassin, huku Namungo ambayo ina mabao manne, matatu yamefungwa na Mrundi Bigirimana Blaise na moja likifungwa na Mtanzania Hashim Manyanya.




Katibu wa Chama cha Soka cha Wanawake Tanzania (TWFA), Somoe Ng'itu (wa pili kushoto), akimkabidhi kombe nahodha wa Shule ya Sekondari ya High View, Sekela Mwakisisile, baada ya kuibuka mabingwa wa Ligi ya Shule za Sekondari kwa wasichana wa umri chini ya miaka 16 (U-16) jijini, Dar es Salaam, ambayo yalidhaminiwa na Kampuni ya KOICA. High View ilishinda penalti 4-3 dhidi ya wenzao wa Jangwani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Tanzania kuweka historia marathon

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA inatarajiwa kuandika historia mpya katika medani ya mchezo wa riadha kimataifa kwa kuandaa mbio za Marathon zinazotambuliwa na Shirikisho la Riadha la Kimataifa 'World Athletics' (WA).

Mbio hiyo itakayojulikana kwa jina la NBC Marathon inatarajiwa kufanyika Novemba 22, mwaka huu jijini, Dodoma na itashirikisha wanariadha 3,000 kutoka ndani na nje ya nchi.

Msemaji wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Tullo Chambo, alisema shirikisho hilo limeingia ubia na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), wa miaka mitano kuanzia mwaka huu 2020 hadi 2024 ili kudhamini mbio hizo.

Chambo alisema ili kuzifanya mbio hizo kukidhi vigezo vya kimataifa, tayari mtaalamu wa kupima njia ambaye anatambulika Chama cha Marathons cha Kimataifa (AIMS), na WA, Givan Wright kutoka Afrika Kusini, ameshakuja nchini kufanya ukaguzi.

Alisema msimamizi huyo atatekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na, John Bayo na Makamu wa Pili wa Rais RT-Ufundi Dk. Hamad Ndee pamoja na viongozi wa Chama cha Riadha Mkoa wa Dodoma.

Akizungumza mara baada ya kuwasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam juzi, Wright mbali na kufurahia kufika Tanzania, alipongeza RT na NBC kwa mipango yao ya kuandaa mbio hizo.

Wright, alisema hii ni fursa muhimu kwa Tanzania kuwa na mbio yenye vigezo vya kimataifa, kwani mbali na kuitangaza nchi kimataifa itawapa fursa wanariadha wa ndani na nje ya kimataifa kupata muda unaotambulika kimataifa.

Aliongeza Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dk. Benelith Mahenge, pamoja na ofisi yake imeahidi kutoa ushirikiano katika kufanikisha tukio hilo la kipekee.

## Kidunda ajipanga kumpiga Mbelwa

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa ngumi za kulipwa kutoka katika Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Selemani Kidunda amesema amejipanga vIzuri kumpiga mpinzani wake, Said Mbelwa katika pambano litakalofanyika Novemba 28, mwaka huu jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kidunda alisema anaamini ataibuka mshindi katika pambano hilo kutokana na maandalizi mazuri na ya muda mrefu aliyofanya.

Kidunda alisema anamfahamu vyema mpinzani wake na anawataka mashabiki wake wasiwe na hofu yoyote kuelekea pambano hilo.

"Naendelea vizuri na mazoezi, nimejipanga na kujiandaa kikamilifu na pambano hilo, naamini nitamchapa mpinzani wangu, naahidi kufanya vizuri, sina lingine," alisema Kidunda.

Alisema anafanya mazoezi magumu kwa lengo la kuuweka sawa mwili wake na anaamini ushindi wa pambano hilo utamweka kwenye nafasi ya kupata pambano la kimataifa.

"Najua Said Mbelwa ana historia nzuri katika ngumi, ila simhofii na badala yake nitamwonyesha kuwa mimi nina uwezo mzuri kuliko yeye," Kidunda aliongeza.

Alisema pambano hilo litakuwa na ushindani kwa sababu linawakutanisha mabondia wenye viwango vizuri.

## Mbeya City sasa yachekelea sare

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutoka suluhu dhidi ya Dodoma Jiji, timu ya Mbeya City imesema imeepokea kwa mikono miwili na kuongeza kuwa haikuwa kazi rahisi kama watu walivyodhani.

Ofisa Habari wa Mbeya City, Shaha Mjanja alisema mechi ilikuwa ngumu na kuongeza sare hiyo kwao si mbaya kutokana na hali waliokuwa nayo kabla ya hapo.

"Kumbuka tumetoka kupoteza mechi nne mfululizo, na sasa tumepata sare mbili mfululizo, huwezi kujua mechi ijayo tunaweza kupata ushindi na tukaendelea kupata ushindi mfululizo," alisema Shaha.

Kiongozi huyo alisema kuwa Dodoma Jiji si timu ya kubeza na imekuwa na matokeo mazuri kwenye uwanja wao wa nyumbani, hivyo wao wanaikubali sare hiyo na kusonga mbele.

"Ukiwa ugenini na timu yenyewe kama Dodoma Jiji, si mbaya, ila kwa sasa tatizo linalotusumbua ni kwa nini hatufungi? Lakini nadhani timu inaimarika na huko mbele tunakokwenda mambo yatakaa sawa," alisema kiongozi huyo.

Pamoja na sare hiyo, bado Mbeya City inaburuza mkia ikiwa na pointi mbili tu kwa mechi sita ilizocheza, ikitoka sare mbili na kufungwa mechi nne.

# Michezo

Jumapili Oktoba 18 2020

Nipashe




## Neymar atakuwa fiti kuikabili Man United

HABARI UK 22

## Azam yajipanga kumlinda Dube

**Na Saada Akida**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Azam FC, wamesema hawana mpango wala mawazo ya kumuuza mshambuliaji wao anayefanya vyema, Prince Dube, imeelezwa.

Dube ambaye anaongoza katika kupachika mabao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, akifunga magoli sita, ameanza kuwindwa na timu mbalimbali baada ya kuonyesha kiwango kizuri kwenye mechi zote sita alizocheza.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulrahman Amin 'Popat' aliliambia gazeti hili jana ni mapema sana kuzungumzia suala la kumuuza mshambuliaji huyo raia wa Zimbabwe ambaye ameitumikia klabu hiyo kwa muda mfupi.

"Hatujapokea ofa yoyote, yanayoendelea katika mitandao ni uongo, Dube amesaini mkataba wa miaka miwili na ndio kwanza ameitumikia klabu kwa miezi miwili tu, lengo letu msimu huu ni kutwaa ubingwa," alisema Popat.

Aliongeza usajili walioufanya msimu huu ulilenga kuipa mafanikio klabu yao na wanashukuru kupata matokeo mazuri kwenye mechi zote sita walizocheza za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Gazeti moja la Zimbabwe limeandika klabu ya Raja Casablanca ya Morocco imeonyesha nia ya kuhitaji huduma ya mshambuliaji huyo ambaye Septemba alitangazwa kuwa mchezaji bora wa mwezi.

Kikosi cha Azam FC kinaendelea na mazoezi kwa ajili ya mchezo wao unaofuata dhidi ya Ihefu FC utakaofanyika Oktoba 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mwanza.



Straika wa Everton, Dominic Calvert-Lewin (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa Liverpool, Virgil van Dijk, katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa jana mchana. Timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2. **PICHA: MTANDAO**

# CHAMA ANA SIRI MOYONI

### ●●● Kiungo huyo anayetajwa Yanga anarejea nchini leo kuendelea na majukumu...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI akiwa bado hajasaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia Simba, kiungo wa kimataifa wa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kutoka Zambia, Clatous Chama, amesisitiza hana mpango wowote wa kujiunga na watani zao, Yanga.

Akizungumza na gazeti hili katika mahojiano maalum, Chama alisema yuko katika hatua za mwisho za kukamilisha mazungumzo na Simba na anaipa nafasi kubwa klabu hiyo kwa hapa nchini.

Chama alisema amekuwa na msimu mzuri ndani ya Simba na hiyo ni moja ya sababu inayomfanya afikirie kuongeza mkataba mpya wa kuitumikia klabu hiyo yenye makao makuu yake Mtaa wa Msimbazi Kariakoo jijini, Dar es Salaam.

Kiungo huyo alisema kwa sasa hajawahi kufikiria kujiunga na Yanga kwa sababu anafurahia maisha ndani ya kikosi cha Simba.

"Kwenda Yanga? Hapana. Ninaamini hivi karibuni nitakamilisha mchakato huo, Simba kuna raha, patamu eeee," alisema kwa kifupi nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya Zambia (Chipolopolo).

Nyota huyo alisema anatarajia kurejea nchini leo baada ya kupata hati mpya ya kusafiria ambayo aliienda kubadilisha nchini kwao.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kikosi chao kitaendelea na mazoezi yake leo asubuhi na maandalizi ya safari ya kuelekea Sumbawanga kuwafuata Tanzania Prisons yamekamilika.

Rweyemamu alisema wataondoka na wachezaji wote ambao wako tayari kwa mechi hiyo, huku majeruhi wakiendelea na programu maalumu za mazoezi chini ya mwongozo wa daktari wao, Yasin Gembe.

Alisema Tanzania Prisons ni moja ya timu zenye vikosi imara na kupata matokeo mazuri inatakiwa kujipanga na kuongeza umakini.

"Tutaondoka Jumatatu na kwenda kupumzika Mbeya, kesho yake (Jumanne), ndio safari ya kwenda Sumbawanga itaanza, tunajua huko tunakwenda kukutana na timu inayotoa changamoto, hatutabweteka, ni mechi itakayokuwa na ushindani," Rweyemamu alisema.

Aliongeza ushindani katika kikosi cha Simba unaongezeka kila siku kwa sababu kila mchezaji anahitaji kuwa sehemu ya wachezaji 18 ambao Kocha Mkuu, Sven Vandenbroeck anawaamini kuelekea mchezo husika.

Aliwataka mashabiki na wanachama wa Simba kuendelea kushirikiana na viongozi ili kufikia malengo ya timu kwa sababu msimu huu ni mgumu zaidi.

"Kuchukua ubingwa wa ligi mara tatu mfululizo si jambo dogo, timu zote 17 zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara zinatuangalia sisi, sio kwa sababu tuna kikosi kizuri, zinataka kutupa changamoto mabingwa watetezi, tunalijua hilo, tumejipanga vizuri kutetea taji," alisema meneja huyo.

Tanzania Prisons iliyohamia kwenye Uwanja wa Nelson Mandela msimu huu, itaikaribisha Simba katika mechi ya raundi ya sita itakayofanyika Jumatano kuanzia saa 10:00 jioni, huku siku hiyo hiyo Yanga ikikutana na 'Maafande' wa Polisi saa 1:00 usiku.

Azam FC yenye pointi 18 baada ya kushinda mechi zake zote sita, ndio vinara wa ligi hiyo wakifuatiwa na Simba, Yanga na Biashara United zenye pointi 13 kila moja.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >